# Nipashe

Alhamisi Agosti 18, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581041

www.ippmedia.com

MWANGA WA JA

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 7

LIKE & FO




NUNEZ AOMBA RADHI KWA KADI NYEKUNDU LIVERPOOL

UKURASA 22


BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,023,154,178

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**NBS** yatangaza ongezeko kubwa la watalii nchini

UKURASA 3

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa



Binti aliyekuwa akiozeshwa ndoa ya utotoni na wazazi wake kwa mahari ya ng'ombe 10 na 200,000/-, akiwa kwenye gari la Jeshi la Polisi pamoja na mama yake mzazi, mshenga na mjomba wake, baada ya ndoa hiyo kuzuiwa na jeshi hilo na maofisa maendeleo ya jamii katika Kijiji cha Manyada wilayani Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Jeshi Polisi lilivyozuia ndoa mtoto kwa mtoto

• **Mama**, mjomba, mshenga watiwa mbaroni... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### DEREVA MBARONI TUHUMA KUUA MKEWE KONDAKTA

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linamshikilia dereva wa daladala, Maarifa Matala (45), mkazi wa Kimara Suka...

## Dereva wa lori lililoua watu 19 asakwa kwa ukaidi

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa (katikati), Mfalme Mswati III wa Eswatini (kulia), wakifuatilia Mkutano wa 42 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) jijini Kinshasa, DRC jana. **Habari ukurasa 4. PICHA: IKULU**

# Abiria alivyojikata koromeo stendi

UK. 2

**MICHEZO** NABI AWAPA AZIZ KI, MORRISON MIEZI 3 UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mcha Hassan Mcha, akizungumza wakati akifungua mkutano wa jukwaa la Taasisi za Kodi Barani Afrika, jijini Arusha juzi. **PICHA: TRA**

# Polisi yazuia ndoa ya mtoto kwa mtoto

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi kwa kushirikiana na maofisa maendeleo ya jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wamezuia ndoa ya ututoni aliyokuwa anafungishwa mtoto mwenye umri wa miaka 15 na mtoto mwenzake mwenye umri wa miaka 17 kwa mahari ya ng'ombe 10 na Sh. 200,000.

Ndoa hiyo ilizuiwa juzi katika Kijiji cha Manyada, Kata ya Usanda, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga baada ya askari polisi na maofisa wa maendeleo ya jamii kufika eneo la tukio.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Deus Mhoja, akizungumza baada ya kuvunja ndoa hiyo, alisema walipata taarifa ya kufungishwa ndoa ya mtoto huyo jana kutoka kwa wasamaria wema ndipo wakapanga mikakati ya kwenda kuizuia.

Alisema mtoto huyo (jina tunalihifadhi) alihitimu darasa la saba mwaka jana katika Shule ya Msingi Manyada na hakuendelea na masomo, hivyo wazazi wake kupata mwanya wa kumwozesha.

"Mtoto huyu sisi kama halmashauri tutaona namna ya kumsaidia ili aendelee na masomo na kutimiza ndoto zake, kwa sababu ni mdogo sana na hatakiwi kuingia kwenye ndoa," alisema.

Mhoja alibainisha kuwa ndani ya mwaka huu halmashauri hiyo imetibua ndoa mbili za watoto, ikiwamo ya mtoto huyo wa Kijiji cha Manyada na mwanafuzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Itwangi.

Alitoa wito kwa wazazi kuacha tabia ya kuendekeza mila na desturi ambazo zimeshapitwa na wakati, zikiwamo za kutothamini watoto wa kike na kuwakatisha masomo yao kwa lengo la kuwaozesha kwa tamaa ya kupata mifugo na fedha.

Mama mzazi wa mtoto huyo (jina tunalo) alisema walimemwozesha binti yao huyo kwa mahari ya ng'ombe 10 na fedha taslimu Sh. 200,000.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto Jeshi la Polisi Wilaya ya Shinyanga, Brihtone Rutajama, aliyekuwa eneo la tukio, alisema katika harusi hiyo waliwakamata bibi harusi (mtoto), mshenga, mama mzazi wa bibi harusi na mjomba wake, huku wahusika wengine wakikimbia baada ya kubaini kuwapo kwa askari polisi na maofisa wengine wa serikali kwenye sherehe hiyo.

**ATOROSHWA**

Wakati hayo yakijiri mkoani Shinyanga, wilayani Sengerema mkoani Mwanza kumeripotiwa tukio la mwanafunzi wa kidato cha tatu mwenye umri wa miaka 19 katika Shule ya Sekondari Kilabela kudaiwa kutoroshwa na vijana wasiojulikana na kumpeleka Kata ya Nyampulukano wilayani humo ili kumwozesha.

Akizungumza kwa Nipashe jana, baba mzazi wa mwanafunzi huyo, Sostenes Berenaldo, alisema alikuwa amesafiri na mke wake na waliporejea nyumbani, hawakumkuta na walipowauliza wadogo zake, wakasema dada yao alibeba nguo na kuondoka.

Berenaldo alisema kuwa siku ya tukio kuna msichana alikwenda nyumbani kwake na kumsaidia mtoto wake kubeba mabegi na kuondoka.

Aliwataka watu wanaotorosha wasichana na kuwakatishia masomo yao, waache kufanya hivyo kwa kuwa wanaharibu ndoto zao.

Ofisa Polisi Jamii Kata ya Nyampulukano, Joyce Pastory, alisema alipewa taarifa na watu kwamba mwanafunzi huyo ametoroshwa na vijana ambao mpaka sasa hawajajulikana.

Aliwataka wazazi kuwa makini na watoto wao kipindi hiki cha likizo maalum ya sensa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mnadani, Rajabu Mgala, aliahidi kulifuatilia suala hilo ili kuhakikisha mwanafunzi huyo anapatikana.

***Imeandaliwa na Marco Maduhu (SHINYANGA) na Eliza Seleman (SENGEREMA)**

# Abiria alivyojikata koromeo stendi

● Asimulia yaliyo nyuma yake

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

ABIRIA aliyekuwa akitoka jijini Dar es Salaam kwenda Dodoma, James Msengi, mkazi wa Mtaa wa Kota mkoani Tabora anayekadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 25 hadi 27, amenusurika kifo baada ya kujaribu kujiua kwa kujichoma kisu kwenye koromeo akiwa ndani ya Kituo Kikuu cha Mabasi Msamvu mjini Morogoro.

Nipashe ilivyofika kituoni huko muda mfupi baada ya kupokea taarifa za tukio hilo, ilishuhudia askari polisi wakimchukua na kumwahisha kijana huyo katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya matibabu huku kukionekana damu eneo la tukio.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo akiwamo mfanyabiashara wa miwa katika kituo hicho, Ibrahim Omary, walisema kijana huyo alifika kwenye eneo la mfanyabiashara huyo na kumpa Sh. elfu mbili ili apatiwe muwa ambao haujamenywa na kumwomba kisu ili aumenye mwenyewe.

"Lakini cha kushangaza baada ya kumpa kisu, hakuchonga muwa, badala yake alikitumia kujichoma kwenye koromeo na kujijeruhi," alisimulia mfanyabiashara huyo.

Shuhuda mwingine, Awadh Athumani, alieleza kushangazwa kumwona abiria huyo ambaye hakufahamu basi alilokuwa amepanda, akiwa ameanguka chini akivuja damu kwa wingi huku kisu kikionekana kwenye koromeo.

"Tulimhoji kwanini ameamua kufanya kitendo kile lakini hakujibu chochote, ndipo askari walioko Kituo cha Mabasi Msamvu wakafika na kumchukua kumkimbiza Hospitali ya Mkoa," alisema.

Nipashe ilifika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro ambako ilidaiwa majeruhi kufikishwa na kuzungumza na Katibu wa Hospitali hiyo na Kaimu Ofisa Uhusiano, Scholastica Ndunga, aliyekiri walimpokea majeruhi huyo majira ya saa 11.30 jioni akiwa amejeruhiwa kooni na akivuja damu nyingi.

"Madaktari walimpatia huduma ya kwanza na sasa amelazwa katika wodi namba moja, akiendelea na matibabu, afya yake inaendelea vizuri, alithibitisha.

Ndani ya wodi namba moja alimolazwa kijana huyo, Nipashe ilizungumza naye ikimshuhudia akizungumza kwa tabu na aliyefungwa bandeji shingoni na eneo alilolala likiwa limetapakaa damu.

Msengi, katika ufafanuzi wake kwa Nipashe kuhusu kilichojiri, alisema alichukua uamuzi huo wa kutaka kujiua kutokana na "kubanwa na hali ngumu kimaisha".

Kijana huyo alisimulia kuwa alitoka Tabora kwenda jijini Dar es Salaam kutafuta maisha, lakini alijiingiza kwenye ulevi, tabia ambayo hakuwa nayo awali na baada ya kuona mambo yanazidi kuwa mabaya, aliamua kuondoka kwenda Dodoma na akiwa Morogoro, likamjia wazo "ni kheri kujiua".

"Baba na mama yangu wanaishi Kota Tabora, walinionya sikutaka kusikia, nikaamini nikifika Dar mambo yangebadilika, lakini kule nikajiingiza kwenye ulevi wa kupindukia na kufanya matendo mabaya.

"Yote haya ni makosa yangu, nikipona, ninarudi Tabora na sitakunywa tena pombe," alijiapiza kijana akiwa na ishara zote za kujutia na kujilaumu kwa uamuzi wake huo wa kutaka kujiua.

Hata hivyo, ndoto zake za kurejea nyumbani kwao Tabora huenda zisitimie kwa kuwa sheria za nchi zinazuia mtu kuua au kujiua, hivyo kuna uwezekano wa kufunguliwa kesi ya jinai hiyo.

Katika mazungumzo yake na Nipashe, Msengi hakutaja basi alikokuwa amepanda lakini alikuwa na tiketi ya kuingia Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli kilichoko Mbezi wilayani Ubungo, Dar es Salaam.

HABARI KITAIFA

# NBS yatangaza ongezeko watalii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), imetangaza ongezeko la watalii kwa kipindi cha miezi saba huku kwa mwezi Julai pekee wakiongezeka kwa asilimia 105.1.

NBS, imeshauri taasisi zinazotoa huduma kwa watalii kuboreshwa zaidi kwa kuwa filamu ya Royal Tour inachangia kuwapo na ongezeko hilo.

Mkurugenzi wa Takwimu za Kijamii wa NBS, Daniel Masolwa, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa takwimu za watalii walioingia nchini Januari hadi Julai mwaka 2022.

Alisema watalii waliotoka nje walioteembelea vivutio mbalimbali vya utalii kwa kipindi hiki wameongezeka hadi 742,133 ikilinganishwa na 456,266 walioingia mwaka 2021 ikiwa ni sawa na asilimia 62.1.

Watalii walioingia kwa mwezi Julai 2022 pekee waliongezeka hadi 166,736 ikilinganishwa na 81,307 walioingia nchini kwa Julai mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 105.1.

"Idadi ya watalii waliongezeka kwa mwezi Julai 2022 ilikuwa zaidi ya mara mbili ya walioingia kipindi kama hicho mwaka 2021, pia kati ya watalii 742,133 walioingia kipindi hiki, 222,449 waliingia kupitia Zanzibar sawa na asilimia 30 ya watalii wote," alisema.

Alibainisha kuwa katika mwezi Julai pekee idadi kubwa ya watalii ambayo ipo kwenye mabano ilikuwa ni kutoka Marekani (17,135), Ufaransa (12,634), Uingereza (8,586), Ujerumani (8,015) na Netherland (5,102).

"Bara la Afrika kwa mwezi Julai idadi kubwa ya watalii walioingia ni kutoka Kenya (16,654), Burundi (7,966), Malawi (5,113), Afrika Kusini (4,335) na Rwanda (4,035)," alisema.

Hata hivyo, alisema watalii kutoka nchi zilizo nje ya Bara la Afrika kwa kipindi cha Januari hadi Julai 2022, walitoka Marekani (51,301), Ufaransa (47,403), Ujerumani (30,817), Poland (29,004) na Uingereza (28,275).

Mkurugenzi huyo alisema kwa Bara la Afrika watalii waliopokewa kwa kipindi hiko ni Kenya (86,220), Burundi (54,577), Malawi (27,079), Uganda (21, 080) na Afrika Kusini (20,868).

"Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye vivutio vingi na vizuri vya utalii, ambavyo vilikuwa havijulikani sana. Kwa sasa idadi kubwa ya watalii wanaoingia nchini ni matokeo ya kazi nzuri na iliyotukuka iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, kupitia filamu ya Tanzania the Royal Tour iliyozinduliwa," alisema.

Alisema filamu hiyo imeleta mapinduzi makubwa katika sekta ya utalii na kwa sasa Tanzania inashuhudia ongezeko kubwa la watalii.

# Dereva lori lililoua asakwa kwa ukaidi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU moja baada ya lori kuyagonga magari matatu na kusababisha vifo vya watu 19 na kujeruhi wengine 29, Jeshi la Polisi nchini limetangaza operesheni kabambe ya kuwashughulikia madereva wote wa malori wanaokiuka Sheria za Usalama Barabarani.

Jeshi hilo limesema kabla ya dereva wa lori kusababisha madhara hayo, alisimamishwa na maaskari, lakini alikaidi na kuendelea na mwendokasi huku kadri lilivyokuwa likishuka kwenye mteremko huo kasi ikiongezeka.

Lori hilo lililokuwa limesheheni mchanga wa dhahabu lilifeli breki juzi katika eneo la Shamwengo na miongoni mwa magari yaliyogongwa ni basi la abiria mali ya Kampuni ya Super Rojas linalofanya safari zake kati ya mikoa ya Mbeya na Njombe.

Mkuu wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Kamishna wa Polisi, Awadh Juma Haji na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Wilbroad Mutafungwa walifika jana katika eneo la tukio kwa ajili ya kufanya ukaguzi.

Maofisa hao walikagua eneo hilo na kubaini kwamba gari la abiria liliburuzwa umbali wa zaidi ya futi 250 kutoka barabarani, gari ndogo aina ya Benz liliburuzwa umbali wa zaidi ya futi 100 kutoka barabarani na yote yalitumbukia korongoni.

Kamanda Awadh Juma Haji, alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe na ukaidi wa dereva wa lori hilo ambaye anadaiwa kuwa alikuwa anaendesha kwa mwendokasi kwenye eneo ambalo haliruhusiwi.

Alisema tochi ya maaskari wa Kikosi cha Usalama Barabarani waliokuwa katika eneo la ukaguzi ilibaini dereva huyo alikuwa anaendesha gari hilo kwa mwendokasi wa zaidi ya kilomita 60 kwa saa kwenye eneo ambalo linatakiwa kuwa na mwendokasi wa kilomita 50 kwa saa.

Hata hivyo, alisema kabla ya kusababisha madhara hayo dereva huyo alisimamishwa na maaskari, lakini alikaidi.

"Dereva huyo baada ya kusababisha madhara haya alitoroka na kutokomea kusikojulikana, sasa tunaendelea kumtafuta ili achukuliwe hatua za kisheria, bahati nzuri ni kwamba kampuni ya gari hiyo imeshajulikana," alisema Kamanda Awadh Juma Haji.

Kutokana na mazingira hayo, Kamanda Haji alisema jeshi hilo litaanza kuwachukulia hatua madereva wote wanaokiuka sheria za usalama barabarani.

Katika hatua nyingine Kamanda Haji alisema katika eneo hilo ajali nyingi zinatokea kutokana na kutokuwapo kwa alama za usalama barabarani hasa ambazo zinaonyesha mteremko mkali na daraja hali ambayo inawafanya madereva wengi kushindwa kuchukua tahadhari. Vilevile, alisema katika eneo hilo barabara ni nyembamba na kufanya kuwa vigumu madereva kujiokoa wakati magari yanapowashinda na kuomba Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) kuipanua na kuweka alama.

Alisema kwa sasa serikali kupitia TANROADS imeanza kujenga kituo cha kukagua magari kabla hayajaanza kushuka kwenye mteremko huo ili kupunguza madhara ya ajali zinazotokea.

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

## TAARIFA YA MAUZO YA NYUMBA ZA MEDELI JIJINI DODOMA

1. Katika muendelezo ya kuwezesha Watanzania wengi zaidi kumiliki nyumba za makazi, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linatangaza rasmi mauzo ya nyumba zilizopo eneo la Medeli Jijini Dodoma. Nyumba hizo zipo ndani ya majengo ya ghorofa ya kisasa na zimekamilika zikiwa na huduma zote muhimu za maji, umeme, maeneo ya michezo na maegesho ya magari. Sifa za ziada za nyumba hizo ni kuwa na eneo maalum la kukusanyia taka.
2. Nyumba zipo katika eneo tulivu la Medeli Jijini Dodoma takriban kilomita moja kutoka katikati ya Jiji na karibu kabisa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Uwanja wa Ndege, Stesheni ya Reli na huduma mbalimbali za kijamii. Nyumba zipo chache za kuuzwa kwenye majengo matatu ya ghorofa 4. Usalama katika nyumba hizo umezingatiwa kwa wakazi na wanunuzi kwa kuweka uzio mkubwa.
3. Kila nyumba ina vyumba vitatu vya kulala, kimoja kati ya hivyo kinajitegemea, sebule iliyoungana na eneo la kula chakula, choo cha umma na jiko kubwa la kisasa. Nyumba hizo zina ukubwa wa mita za mraba 117.2
4. Kila nyumba itauzwa kwa bei ya **TZS 199,870,670** bila kodi ya ongezeko la thamani (VAT) Tunawahamasisha na kuwakaribisha Watanzania wote walio nchini na wanaoishi nje ya nchi wafanye mawasiliano na Ofisi zetu za Makao Makuu ya Shirika, Ofisi za Mikoa, au kupitia baruapepe na kukamilisha taratibu mapema kwa ajili ya kuweza kununua nyumba.
5. Mauzo haya ya nyumba hizi ni mwendelezo wa mauzo ya nyumba za miradi ya NHC yanayolenga kutimiza malengo ya Mpango Mkakati wa Shirika wa miaka kumi (2015/16 – 2024/25).
6. Ukiwa mdau na mnunuzi mtarajiwa, ama una ndugu/rafiki anayehitaji kununua nyumba hizo, tafadhali wasiliana na Kitengo cha mauzo kwa Simu Namba **0736 114433;** baruapepe: **sales@nhc.co.tz** na pia tembelea tovuti ya Shirika **www.nhc.co.tz** kwa maelezo zaidi.

**IMETOLEWA NA:**

**KITENGO CHA HABARI NA UHUSIANO**
**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**

216999901

# Ajenda chakula yatawala mkutano SADC

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wamesisitiza umuhimu wa bara la Afrika kujitosheleza kwa chakula.

Suala hilo lilikuwa moja ya ajenda zilizotawala katika Mkutano wa 42 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa SADC uliofanyika Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC). Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa miongoni mwa viongozi waliohudhuria mkutano huo.

Katika mkutano huo, Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, ambaye alishiriki kwa mara ya kwanza tangu alipochaguliwa mwaka jana, alisema lengo la mkutano huo ni kusaidia viwanda, uchakataji wa mazao ya kilimo na utangamano wa pamoja katika sekta mbalimbali na kuleta fursa kwa wananchi.

"Afrika inakabiliwa na uhaba wa chakula kwa sababu kuna tatizo kwenye vita vya Russia na Ukraine na matatizo mengine ya ndani ambayo lazima tuyaangalie kabla ya kuangalia kwingine na kuhakikisha watu wetu wanapata chakula cha kutosha na kuwa na usalama," alisema.

Rais Hichilema (Pichani) pia alisema ni muhimu kwa nchi za SADC kuongeza uchakataji na thamani kwenye uzalishaji hasa sehemu ya chakula.

Alisema kwa sasa umeme utokanao na nishati jadidifu kwa ajili ya magari ni muhimu katika soko hilo la thamani na kuleta teknolojia na kubadilisha malighafi hizo kuwa bidhaa imekuwa changamoto katika miongo kadhaa.



Hichilema alisema pia ni muhimu kuwekeza kwenye rasilimali watu, elimu, afya, lishe ni mambo ya msingi kwenye ukanda huo.

Aidha, alisema katika ukanda huo ni jukumu lao kuhakikisha elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi sekondari na kuendelea hadi vyuo vikuu, pamoja na ulinzi na usalama ambao lazima upewe kipaumbele katika kuongeza ajira.

Aliwashukuru nchi zote kwa msaada wao katika uchaguzi uliofanyika Agosti, mwaka jana kwa sababu walikuwa wana changamoto mbalimbali za kidemokrasia.

Naye Rais wa DRC, Félix Tshisekedi, alisema maandalizi ya mkutano huo ni wakati mgumu lakini uwapo wao unachangia kukua wa jumuiya yao.

Katibu Mtendaji wa SADC, Elias Magosi, alisema mkutano huo ni wa kwanza tangu ameajiriwa na kwamba ameona SADC ni umoja wenye utangamano wa kikanda.

"Baada ya kuchukua nafasi hii niliwapokea na kuwapa taarifa kuhusiana na utekelezaji wa shughuli zetu kama sekretarieti na juhudi zetu za kuufanyia kazi utengamano wa kikanda, ninaahidi na juhudi hizi kuhakikisha," alisema.

Alisema kwa kipindi cha ushirikiano huo wamefikia malengo baada ya kupitisha itifaki, matamko na mipango mikakati mbalimbali.

"Ni wakati muafaka wa kutumia vyombo mbalimbali ili kuruhusu utengamano wa kikanda pamoja na ukuaji wa viwanda katika ukanda wetu, kuhakikisha tunakuwa na ushirikiano, kuainisha mikakati yetu na sera ili utangamano wa kikanda unasonga mbele," alisema.

Pia alisema watahitaji kuweka juhudi nyingi zaidi kuhakikisha uchumi katika nchi zinakuwa na ushirikiano ili kukabiliana na matatizo mbalimbali ikiwamo usalama ambao umebaki salama kwa ujumla.

Alisema suala la unyanyasaji wa kijinsia linaendelea kuwa tatizo na kuathiri maendeleo ya kijamii, na kwamba asilimia 71 linaathiri wanawake na asilimia 23 ni wanaume.

Pia alisema hilo linadhihirisha kwamba ukatili dhidi ya wanawake unavunja moyo wa wanawake katika ukanda huo na hivyo wanahitaji juhudi za pamoja, ili kuondokana na ukatili huo.

Kuhusu usalama na uhakika wa chakula, alisema wakuu hao wameona umeongezeka kutoka asilimia saba hadi asilimia 34, huku akitaka kipaumbele baina ya nchi hizo ili kuwa na ziada ya chakula.

**MAMBO YA KUFANYIKA**

Magosi alisema ukanda huo unatakiwa kuweka kipaumbele ukuaji wa kiuchumi, ili kuvutia wawekezaji na kufanyia kazi pungufu la nishati ambalo nchi nyingi zinakabiliwa nalo.

Pia alisema ukanda huo unakabiliana na upungufu katika ujenzi wa miundombinu, kuendeleza uzalishaji, kuboresha mazingira ya biashara na kutumia mfuko wa SADC, ili kuleta rasilimali za kifedha na kusaidia utekelezaji wa miradi hasa wanapokabiliwa na upungufu wa fedha nchi wanachama.

Kadhalika aliomba ushirikiano wa viongozi hao katika kuvutia rasilimali zinazotakiwa, ili kusaidia kusonga mbele kwenye utangamano wa kikanda na kutumia faida ya kuwa na idadi kubwa ya vijana.

21700802

UN WOMEN
United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women

CALL FOR PROPOSAL

The United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women (UN Women) Tanzania is pleased to announce a Call for Proposals from organizations with a track record in human rights, women's rights and gender equality to implement creative and innovative strategies, approaches, and interventions to transform gender norms, discriminatory behaviour and practices to promote women and girls' voices, meaningful participation, leadership, and economic rights at the local level (ward, village, streets, vitongoji, e.t.c) in the selected district councils of Dar es Salaam, Coast, Lindi, Mtwara , Arusha and Singida.

The organizations should have a base and previous experience in implementing projects in the respective regions. If it's a national organization that does not have experience in the respective regions, but plans to expand its projects to the WLER Project regions building on learnings from the implantation of similar projects, it should indicate previous collaboration with other human and women's rights organizations and networks including those promoting the rights of young women and women with disabilities; and duty bearers, including local government actors and community facilitators in the respective regions to deliver on the project objectives. The organizations should also demonstrate experience working with opinion makers such as community and traditional leaders, religious leaders, male gender equality and women's empowerment champions, decision-makers, and the media.

The full Call for Proposal (CFP) may be downloaded from:

https://www.unwomen.org/en/about-us/programme-implementation/2022/08/call-for-proposals-unw-esa-tza-2022-001-transforming-gender-norms

The Call for Proposals will be open until **31st August 2022 at 23.59 hrs (EAT) (Tanzanian Time).**

**All proposal MUST be submitted through email cfp.tanzania@unwomen.org with subject line REF: CFP No. UNW-ESA-TZA-2022- 001 on Transforming Gender norms and discriminatory behaviours and practices at local levels to promote women and girls' voices, meaningful participation, and leadership.**

Only **those short listed** will be contacted for further screening and consideration.

**Proposals received after the deadline will not be considered.**

For more information, please email: agness.hanti@unwomen.org by **31st August 2022 at 23.59 hrs (EAT).**

# Dereva mbaroni tuhuma kuua kondakta wake wivu mapenzi

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linamshikilia dereva wa daladala, Maarifa Matala (45), mkazi wa Kimara Suka wilayani Ubungo, kwa tuhuma za kumuua mpenzi wake ambaye alikuwa kondakta wa gari analoendesha.

Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Jumanne Muliro, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini, alisema tukio hilo lilitokea Agosti 16, mwaka huu.

Kamanda Muliro alimtaja kondakta aliyeuawa ni Sharifa Nyamaishwa (31), mkazi wa Kimara Suka, aliyeshambuliwa sehemu mbalimbali za mwili wake.

"Baada ya dereva huyu kutenda tukio hili, alikimbia, Sharifa alifariki dunia baadaye. Polisi baada ya kupata taarifa tulifanya upelelezi na ufuatiliaji wa haraka tukamkamata akiwa mkoani Lindi alikojificha," alisema.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, uchunguzi wa awali umebaini wapenzi hao walikuwa na migogoro inayosababishwa na wivu wa kimapenzi na kusababisha kugombana mara kwa mara na kwamba mwili wa marehemu ulikutwa na majeraha.

Wakati huo, jeshi hilo linamshikilia mfanyabiashara Gamariel Swai (43), mkazi wa Mbezi kwa tuhuma za kuuza spea za magari zilizoibwa kwenye magari ya watu mbalimbali.

Kamanda Muliro alisema duka la mtuhumiwa huyo liko Mtaa wa Songea jijini Ilala, akifafanua kuwa Julai 23 mwaka huu, alipokea taarifa ya wizi wa vifaa vya gari maeneo ya Kivule Bombambili, Ukonga ambako Sifael Msemwa (38), mkazi wa Bombambili aliibiwa vifaa vya gari lake lenye namba za usajili T429 BKK, aina ya Toyota Prado lililokuwa limeegeshwa nyumbani kwake.

Kamanda Muliro alivitaja vifaa hivyo kuwa ni vioo vitatu, power 'window' nne, 'control box' na betri ya gari hilo.

"Baada ya upelelezi Agosti 15 mwaka huu, Swai alikamatwa na upekuzi ulipofanyika kwenye duka lake, walikutwa na vioo viwili, 'power window' nne. Pia tulikamata vifaa vingine vya magari vilivyodhaniwa ni vya wizi kutokana na kutokuwapo maelezo ya kutosha," alisema.

Alivitaja vitu vilivyokamatwa kuwa ni taa za mbele 93 za magari mbalimbali, 'power window' 189 za magari ya aina mbalimbali, vioo 62 za magari, 'show' za mbele saba, za ndani 35, mikono ya milango (vitasa 26), rejeta moja na betri moja.

Kamanda Muliro pia alisema polisi wanaendelea na operesheni kali dhidi ya wanaojishughulisha na matukio ya kihalifu, ikiwamo wizi wa magari na uuzaji wa vifaa vya magari vitokanavyo na magari ya wizi.

***Imeandaliwa na Aisha Kondo (DSJ) na Isiyaka Nyamihasi (TUDARCo)**

# PM atatua mgogoro viwanja Boko Dovya wa miaka 3

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ametatua mgogoro wa ardhi uliodumu kwa miaka mitatu katika eneo la Boko-Dovya, wilayani Kinondoni, jijini Dar es Salaam baina ya Aloyce Mwasuka na Salutari Massawe.

Katika mgogoro huo unaohusisha viwanja namba 393, 395 na 370 kwenye kitalu G (Boko Dovya), njiapanda ya Mbweni, Massawe alijenga ukuta ambao ulikuwa unazuia matumizi ya barabara na kumfanya Mwasuka apitie kwa jirani yake, Oliver Semuguruka (kiwanja na. 395) ili aweze kufika nyumbani kwake.

Akizungumza na watendaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, watendaji wa Wilaya ya Kinondoni katika kikao alichokiitisha jana ofisini kwake jijini Dar es Salaam, Waziri Mkuu alisema ameridhishwa na hatua aliyoichukua Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe ya kusimamia uvunjaji wa ukuta huo ili kupisha eneo la barabara.

"Ninakushukuru Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na timu yako kwa kuchukua hatua tangu jana ili kusimamia haki ya wananchi wasio na uwezo. Haki ni ya kila mmoja, mwenye uwezo na asiye na uwezo. Ile barabara iboreshwe ili wananchi wote wanufaike," alisema.

Alisema hatua hiyo inaenda sambamba na utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyowapa wasaidizi wake akitaka wahakikishe kuwa wananchi hawapati shida kwenye maeneo yao.

Akisisitiza usimamizi wa majukumu yao kwa watendaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Waziri Mkuu amesema: "Nendeni mkasimamie masuala ya ardhi ili watendaji wa serikali nao wafanye kazi nyingine za kuwahudumia wananchi. Lazima tufanye mifumo isimamiwe ili kazi nyingine ziendelee," alisisitiza.

Mapema, akitoa taarifa kwa Waziri Mkuu, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, alisema eneo hilo limeainishwa kwenye ramani ya mipango miji ya mwaka 2002 (TP 2002) na kwamba Massawe alinunua eneo hilo mwaka 2004 na akalipima mwaka 2005, wakati Mwasuka alinunua eneo lake mwaka 2005 na akalipima mwaka 2006.

"Katika upimaji wao kila mmoja alitumia mpimaji wake, lakini coordinates zinaonesha kuwa kuna barabara katikati yao na ramani zao pia zinatambua barabara hiyo. Wote wawili walipaswa kuheshimu michoro ya mipango miji ambayo ni michoro mama," alisema Mkuu huyo wa wilaya.

Naye Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam, Idrissa Kayera, alimweleza Waziri Mkuu kwamba licha ya kuwa ramani zote mbili zimeitambua barabara hiyo yenye upana wa mita 12, Massawe aliamua kujenga ukuta upande mmoja katika eneo lake ambao uliziba eneo hilo la barabara na hivyo kufunga barabara inayotenganisha viwanja namba 393, 395, 370, 391,390 na 369.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwan Kikwete, alisema wizara itaendelea kusimamia migogoro yote iliyopo na kuweka mpango wa kuishughulikia.

Mwasuka alimshukuru Waziri Mkuu, Naibu Waziri, Mkuu wa Wilaya na timu yao ya watendaji kwa kutatua migogoro huo na akaomba timu hizo mbili ziendelee kushirikiana ili kuwasaidia wananchi wengine wasio na sauti. Massawe hakufika kwenye kikao hicho kwa sababu ya changamoto ya kiafya.

# Shaka aonya madeni ya makandarasi

**Na Beatrice Shayo,** KALIUA

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amewataka wakurugenzi na wakuu wa wilaya kuhakikisha makandarasi wanapoacha au kumaliza kazi wasiache madeni kwa wananchi.

Shaka aliyasema hayo jana wakati akikagua mradi wa ujenzi wa barabara ya Ushokola hadi Kaliua, mkoani Tabora, yenye urefu wa kilometa 2.1 inayojengwa kwa kiwango cha lami.

Awali, wananchi hao walimlalamikia kitendo cha mkandarasi kuvunjiwa mkataba na halmashauri bila kupatiwa malipo wanayodai katika kipindi cha miaka mitatu na kumwomba awasaidie kupatiwa haki yao.

Baada ya kusikiliza kero za wananchi hao, Shaka alizitaka halmashauri zote nchini kuwasimamia makandarasi wanaowapa nafasi ya kutoa huduma iwe ujenzi wa barabara, vituo vya afya au huduma katika halmashauri kuhakikisha haki za wananchi wanyonge zinalindwa.

Shaka alisema kuna tabia imejengeka nchini kwa makandarasi kutoa kazi kwa wananchi wa ngazi ya chini inapotokea wameharibu kazi hawawalipi.

"Jambo la kwanza simamie haki za wananchi wanyonge haiwezekani mkandarasi anapewa kazi analipwa na halmashauri anaharibu kazi anaondoka anaacha mzigo wa madeni. Hii si sahihi na wala si ubinadamu," alisema Shaka.

"Niwaombe ndugu zetu mliopewa dhamana katika hizi halmashauri kuhakikisha mkandarasi anapoacha kazi hana madeni kwa wananchi na jambo la pili haki za binadamu kwa wale waliokuwa wanatoa huduma zinapatikana ikiwamo wale vibarua wanaofanya kazi," aliongeza.

Kiongozi huyo alisema endapo wakitekeleza jambo hilo itasaidia kwa kiasi kikubwa kujenga uimara na kutokudumaza hali za wananchi.

"Huyu mama amefanya kazi kwa miaka mitatu katika mazingira magumu halafu mkandarasi ameshindwa kazi anaondoka anaacha mzigo wa madeni nawaomba viongozi mkaliangalie hili jambo kwa umakini hakuna mkandarasi kuacha kazi bila kulipa madeni kwa wananchi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Paul Chacha, alisema kwa kushirikiana na watendaji wenzake, wataongeza umakini wa kusimamia makandarasi ili wananchi wasinyimwe haki zao.

Alisema maagizo yote ambayo wamepatiwa wataenda kuyafanyia kazi kwa kushirikiana na viongozi wenzake katika kuhakikisha maendeleo yanawafikia wananchi.

Wakati huo huo Shaka alitembelea ujenzi wa shule katika kijiji cha Kondamoyo alisema atakwenda kuzifanyia kazi changamoto zote alizopatiwa kwa kuziwasilisha ngazi kuu ya serikali hasa ombi la mgawanyo wa halmashauri.

Hata hivyo, Shaka aliwataka vijana kutumia fursa za uwekezaji kwani Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha nia kwa kuamua kuwawezesha na mzunguko wa fedha upo vizuri umefika hadi ngazi ya chini.

"Inaonekana bado vijana hawanufaiki katika fursa za kujiajiri kubwa anayoifanya Tanzania kuhakikisha fedha ziwaongezee vipato ni vyema viongozi waone umuhimu wa kuhakikisha fedha zinawafikia vijana," alisema.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

## BESIX BALLAST NEDAM (BBN) LIMITED
## TANGAZO LA KAZI – AFISA UHUSIANO WA JAMII (CLO)

MKANDARASI wa Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi wa Gati na Mizigo katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki ( EACOP ) linakaribisha maombi ya **nafasi ya Afisa Uhusiano wa Jamii (CLO).**

| | |
|---|---|
| Mradi | EACOP – Ujenzi wa Gati na kituo cha kupakia mafuta ghafi |
| Mwajiri | Besix Ballast Nedam Limited (BBN) |
| Mahali pa Kazi | Chongoleani – Tanga |
| Cheo cha Nafasi | Afisa Uhusiano wa Jamii (CLO) |
| Inaripoti Kwa: | Kiongozi wa shughuli za Kijamii wa BBN |
| Muda wa Ajira | Oktoba 2022 hadi Oktoba 2023 (mwaka 1) |
| Aina ya Kazi | Wakati wote |
| Mzunguko wa Kazi | Utatangazwa (TBC) |
| Idadi ya Wagombea | Utatangazwa (TBC) |
| Siku/Saa za Kazi | Siku 6 kwa wiki (kuzingatia kanuni za kazi za Tanzania) |

**Wigo wa kazi.**
Afisa Uhusiano wa Jamii atawajibika kwenye utekelezaji wa vipengele muhimu vya Mpango wa Ushirikiano wa Wadau wa BBN na ndiye kiunganishi cha msingi na jumuiya zilizo karibu zaidi na shughuli za BBN. CLO ataripoti kwa Kiongozi wa shughuli za Kijamii wa BBN. Pia, atahakikisha mawasiliano kati yake na Meneja wa Ujenzi wa BBN kuhusu maendeleo ya kazi na masuala yote ya Kazi za Ujenzi na kuzijulisha jumuiya zinazozunguka Mradi, mambo yote yatokanayo na shughuli za BBN.

CLO atawakilisha na kuunganisha shughuli za BBN na jamii pamoja Serikali kupitia mamlaka za serikali za mitaa; CLO atapaswa kujua mpangilio wa shughuli za BBN na kufahamu, namna na lini shughuli husika zitafanyika na jinsi zitakavyosimamiwa kisha atawasilisha kwa jamii inayozunguka mradi na wadau wengine wa mradi taarifa husika. CLO atakuwa na jukumu la kurekodi na kuripoti malalamiko yanayohusiana na Mradi yaliyotolewa na wanajamii au wadau wa Mradi.

Nafasi ya CLO ni ya muda wote wa Mradi, itayotegemea mpangilio wa shughuli za Ujenzi na eneo la makazi litakuwa Tanga mjini.

**Majukumu ya kazi**
- Kukuza uelewa wa wadau wa ngazi ya Wilaya, Kata, Kijiji na Kaya jinsi wanavyoweza kuathiriwa na shughuli za BBN.
- Kukuza uelewa wa shughuli za ujenzi za BBN, maeneo ya kazi (maeneo yatakayoathirika moja kwa moja na ambayo hayataathirika moja kwa moja) na aina za ushirikishwaji wa jamii unaohitajika kisha kuzijulisha jamii kuhusu mpangilio wa kazi za BBN.
- Kutekeleza mpango kazi wa Kushirikisha Wadau wa BBN
- Kuunganisha mwakilishi wa Ujenzi wa Mradi wa BBN na Afisa uhusiano wa Jamii (CLO) wa EACOP kuhusu shughuli za ujenzi za BBN
- Kutengeneza na kushiriki kusambaza taarifa za Mradi wa BBN kwa Afisa uhusiano wa Jamii (CLO) na Jumuiya zinazozunguka Mradi.
- Kuitaarifu BBN kuhusu masuala ya jumuiya husika, maoni yao na kutoa angalizo ya hatari / athari zinazoweza kutokea kwenye Mradi ili BBN iweze kuchukua hatua.
- Kunakiri na kuripoti maswali ya wajumuiya na masuala yanayohusiana na Mradi, kisha kushiriki katika kuandaa na kutoa majibu husika, kwa wakati.
- Kutekeleza Mpangokazi wa EACOP wa Usimamizi wa Malalamiko wa Mradi na kuratibu utaratibu wa kutatua kero zinayohusiana na shughuli za BBN.
- Kuweka rekodi na taarifa zote za ushiriki wa washikadau, pamoja na kutunza kumbukumbu za mikutano, rejista za mahudhurio, picha, na nakala za ripoti zilizoandikwa; na kusimamia hifadhidata ya nakala zote ngumu/laini kwa kushirikiana na EACOP.
- Kusimamia rejista ya/na urekodi maswala yote ya washikadau, masuala na maoni yoyote ya washikadau yanayohusiana na shughuli za ujenzi wa BBN ili kuchukuliwa hatua na Kiongozi wa shuhuli za Kijamii wa BBN.
- Kutoa taarifa na ripoti za ushiriki wa wadau wa ujenzi za kila siku, kila wiki, na kila mwezi kama inavyohitajika.
- Kusaidia shughuli za ujenzi za BBN na shughuli za ushiriki kwa Jamii kama inavyohitajika akishirikiana na Kiongozi wa shughuli za Jamii wa BBN na Meneja wa Ujenzi wa BBN.

**Sifa za Kazi, Uzoefu na Ustadi**
**Muombaji awe na sifa zifuatazo:**
- Raia wa Tanzania mwenye Shahada ya Kwanza katika sayansi ya jamii, sosholojia, sayansi ya mazingira, Mahusiano ya Umma, mawasiliano au taaluma nyingine zinazoshabihiana.
- Uwezo wa kuongea na kuandika, Kiingereza na Kiswahili.
- Angalau miaka 5 ya uzoefu wa kufanya kazi na washikadau na kuandaa mikutano ya jumuiya za vijijini.
- Angalau miaka 3 ya uzoefu katika shughuli za ujenzi, sifa ya ziada.
- Asiwe na historia ya kufungwa au kujihusisha na uhalifu / shughuli zinazohusiana na magenge ya kiharifu.
- Uzoefu katika kufanya shughuli na ushirikishwaji na mamlaka (serikali za mitaa, vijiji, manispaa, taasis mbalimbali n.k; ) pia afahamu itifaki zinazohusiana na shughuli husika.
- Kiwango cha juu cha ustadi-binafsi na uwezo uliothibitishwa wa kukuza na kudumisha uhusiano mzuri, kwa wigo mpana, na washikadau ikiwa ni pamoja na kiwango cha juu cha Usiri, Diplomasia na uwezo wa Kudhibiti migogoro na kutafuta makubaliano, inahitajika.
- Kiwango cha juu cha ushirikiano na uwezo wa kupanga na malengo, itapewa kipaumbele
- Uwezo uliothibitishwa wa kufanya kazi kwa kujitegemea bila shurti, kukamilisha kazi zinazohitajika kwa wakati na kuwasilisha ripoti ndani ya muda,
- Uandishi bora wa ripoti na ustadi wa uchambuzi unahitajika, pamoja na umakini kwenye mambo munimu,
- Ustadi wa kutumia kompyuta pamoja na matumizi ya programu za MS Excel, MS Word, MS PowerPoint, MS Teams na uzoefu wa kutumia programu ya usimamizi wa data na takwimu.

**Jinsi ya Kutuma maombi**
Maombi yote yatumwe kwenye anuani ya barua pepe, **procurement@bbnjv.com (Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20) mnamo au kabla ya tarehe 1 Septemba 2022, Saa 6 mchana kwa saa za Tanzania.**

**TAFADHALI ZINGATIA,** ikiwa hutawasiliana nawe ndani ya wiki 2 baada ya uchapishaji huu, zingatia kuwa ombi lako halijafaulu.

2170000202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Polisi watekeleze wajibu kudhibiti ajali barabarani

**WIMBI** la ajali limeendelea kutikisa katika maeneo mbalimbali nchini na kusababisha vifo vya mamia ya watu huku wengine wakijeruhiwa na kupata ulemavu wa kudumu.

Licha ya kusababisha madhara hayo, ajali hizo pia zimekuwa chanzo cha kupotea kwa nguvu kazi ya taifa, uharibifu wa magari na hasara katika kampuni za bima.

Juzi, mathalani, watu 19 walifariki dunia na wengine kujeruhiwa baada ya lori lililokuwa limesheheni mchanga wa dhahabu likitokea Chunya mkoani Mbeya kwenda Dar es Salaam, kufeli breki katika mteremko wa Inyala jijini Mbeya na kuparamia magari matatu.

Magari hayo yaliyogongwa na lori hilo, ni pamoja na basi moja la abiria linalofanya safari kati ya Mbeya na Njombe na idadi kubwa ya waliopoteza maisha walikuwa katika basi hilo.

Licha ya sababu zinazoelezwa kila ajali inapotokea kuwa baadhi ya magari kufeli breki, vyanzo vingine vimekuwa vikitajwa kuwa ni mwendokasi wa madereva, matumizi ya vilevi na ubovu wa magari.

Katika ajali ya juzi, taarifa mpya zilizotolewa na polisi jana zilibainisha kuwa lori lililosababisha maafa hayo lilikuwa bovu na hilo lilibainika baada ya polisi kikosi cha usalama barabarani kufanya ukaguzi. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, dereva wa lori hilo ambaye alikimbia baada ya kusababisha ajali, anadaiwa kukimbia na sasa anasakwa ili achukuliwe hatua za kisheria.

Kutokana na sababu hiyo, kunaibuka maswali mengi ambayo baadhi yanakosa majibu. Moja ya maswali hayo ni, je, ilikuwaje polisi wakaruhusu gari hilo kuendelea na safari ilhali limebainika kuwa ni bovu? Swali la pili, ni kwa nini dereva akaidi mbele ya polisi wakati chombo hicho kina mamlaka ya kuchukua hatua za kulisimamisha kuendelea na safari hadi kasoro zilizojitokeza zitakaporekebishwa?

Ukakasi uliomo katika maswali hayo, unatokana na ukweli kwamba Jeshi la Polisi hususan Kikosi cha Usalama Barabarani, limekuwa likitajwa mara kwa mara kuwa ni moja ya taasisi ambazo zimekithiri katika tuhuma za rushwa. Kwa msingi huo inawezekana kuna mazingira ya rushwa yalikuwapo hadi gari hilo kuendelea na safari ilhali lilibainika kuwa ni bovu.

Kwa msingi huo, kuna mazingira yanayojionyesha kuwa polisi kwa namna yoyote ile wanahusika katika ajali hiyo. Tunasema hivyo kwa sababu taarifa waliyoitoa imebainisha kuwa dereva alikaidi! Dereva anakaidi vipi mbele ya chombo cha dola na akaachwa bila kuchukuliwa hatua?

Kwa mazingira hayo, ni wakati mwafaka sasa kwa Jeshi la Polisi hususan kikosi chake cha usalama barabarani kujitathmini na kurejea katika mstari wake na kutekeleza majukumu yake ili kulinda maisha ya watu ambayo kwa sasa yako hatarini kutokana na ajali ambazo zimetamalaki na zinatokea kila uchao. Licha ya kutekeleza majukumu ipasavyo, pia askari walioruhusu gari hilo kuendelea na safari pamoja na kuwa bovu, wachukuliwe hatua.

Ni imani kwamba iwapo Jeshi la Polisi litasimamia kanuni, taratibu na sheria zinazosimamia usalama barabarani, ajali ambazo zimekithiri sasa zitapungua kwa kiasi kikubwa. Ni vyema polisi wakatekeleza wajibu wao kama ulivyoainishwa kwa mujibu wa sheria, kwa maana ya usalama wa raia na mali zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kama 'kiroba' kilivyokoma ukatili utokomezwe sasa

Na Sabato Kasika

**IWAPO** serikali ilikomesha ufungashaji wa pombe kwenye mifuko ya nailoni almaarufu 'kiroba' ni wakati wa kubuni na kuibua mikakati mahsusi ya kukomesha ukatili wa kijinsia na kuwa historia.

Kuna haja kwa sababu matukio ya ukatili 11,499 yaliripotiwa kuanzia Januari hadi Desemba mwaka jana, huku ubakaji ukiongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya visa 5,900. Kingine kinachofuata ni mimba za utotoni 1,677 na ulawiti matukio 1,474, huku ikielezwa kuwa matukio mengi hayaripotiwi kwenye vyombo vya dola.

Ni taarifa ya hivi karibuni ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anayetaja mikoa inayoongozwa kwa ukatili kuwa ni Arusha, Tanga, Shinyanga na Mwanza.

Kwa taarifa hiyo, ni wazi kwamba kila mmoja ana jukumu la kufanya, kwa ajili ya kukabiliana na vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia na kuvipunguza.

Kila mmoja akishiriki katika vita dhidi ya vitendo vya ukatili huo, jamii inaweza kubadilika na kuchukua hatua za kuvikomesha au kutoa taarifa kwa vyombo vya dola, ili hatua za kisheria zichukuliwe kwa watuhumiwa.

Waziri Gwajima, anasema serikali imejizatiti kumaliza vitendo vya ukatili kwa kutoa adhabu kali kwa wahusika, lakini kuhamasisha jamii na anaomba ushirikiano wa Watanzania ili kukomesha vitendo hivyo.

Kwa ombi hilo la serikali ni vyema hilo likafanyika ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za kuwapo kwa vitendo hivyo au hata viashiria vyake kabla havijasababisha madhara kwa watoto wa kike na kiume.

Katika jitihada za kukabiliana na vitendo hivyo, Waziri anaeleza kuwa milioni 119. 6 zimetengwa kwa ajili ya kampeni iitwayo "Twende Pamoja, Ukatili Tanzania Sasa Basi", yenye lengo la kujenga uelewa kwa jamii kuhusu usawa wa kijinsia na kupinga ukatili.

Hatua hiyo imekwenda sambamba na kampeni nyingine ya kupinga na kutokomeza ukatili inayoitwa Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA), ambapo anafafanua kuwa kufikia Julai mwaka huu, watu 8,000 walikuwa wameshajiunga nchini kote.

Kutokana na jitihada hizo zinazofanywa na serikali, inaelezwa kuwa imesaidia kuongezeka kwa idadi ya watu wanaotoa taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia kwa vyombo vya dola kwa kipindi cha mwaka 2020/21 ambapo matukio 20,025 ya ukatili yaliripotiwa ikilinganishwa na matukio 18,270 yaliyofikishwa polisi mwaka 2019/20.

Pia, imesaidia kuanzishwa kwa madawati ya jinsia yanayoshughulikia mashauri ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kufikia 420 katika vituo vya polisi na madawati mengine 153 katika Jeshi la Magereza.

Vilevile, zimeanzishwa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto 18,186 kitaifa, mkoa, wilaya, kata na kwenye baadhi ya mtaa, vijiji na vitongoji, zinazoendelea kufanya kazi.

Jambo la muhimu kama nilivyoeleza awali, ni kila mmoja wetu kwa nafasi yake kupiga vita vitendo hivyo, kama njia mojawapo ya kushirikiana na serikali, ili kuhakikisha jamii inaishi kwa amani bila vitendo hivyo.

Ikumbukwe kuwa, ukatili huo unatajwa kuwa ni kitendo ambacho mtu yeyote anaweza kufanyiwa, awe mwanamke au mwanaume, kwa lengo la kumdhuru ama kumuumiza kisaikolojia, kimwili, kiafya, kingono na kiuchumi.

Kwa mfano ukatili wa kimwili, ni pamoja na kupigwa, kusukumwa, kuporwa, kukeketwa na kadhalika. Lakini pia upo ukatili wa kisaikolojia, ambao ni vitendo anavyofanyiwa mtu ili kumwathiri kiakili.

Vitendo hivyo vinajumuisha kutukanwa, kufokewa, kutengwa, kudhalilishwa kwa maneno, vitendo vya ishara, gubu, kusingiziwa, kuaibishwa au kuhukumiwa bila kuwa na kosa.

Upo pia ukatili wa kingono, ambao unahusisha kubakwa, kukosewa uaminifu, kufanyiwa ngono bila kinga, kushikwa sehemu za mwili bila ridhaa, lakini pia kuna ukatili wa kiuchumi unaotokana na kukosa sauti katika mali inayokuhusu.

Ukatili huo wa kiuchumi unahusisha pia kufanyishwa kazi kwa malipo kidogo, kutomiliki mali inayokuhusu, usafirishwaji wa wanawake na watoto kwenda kufanyishwa kazi bila ridhaa yao.

Vilevile, kuna ukatili wa kiafya ambao unaambatana na kukosa haki ya uzazi ya kujifungulia hospitalini, mume kumnyima mke pesa ya kwenda hospitali. Mume kumzuia mke kutumia uzazi wa mpango.

Ikumbukwe unagusa matumizi ya mipira ya kiume (kondomu), mwanaume kutokuwa tayari kutumia mpira huo, wanaume kupimwa VVU na UKIMWI na kumficha mkewe matokeo au kumtuhumu kumwambukiza.

# Ridhiwani awaonya maofisa ardhi kuhodhi viwanja na kuibua migogoro

**Na Idda Mushi,**
MOROGORO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amewaonya maofisa ardhi nchini kujilimbikizia na kuhodhi viwanja, hivyo kugeuka kuwa sehemu ya migogoro ya ardhi katika maeneo yao ya kazi.

Ridhiwani alisema hayo jana alipofanya ziara mjini hapo kukagua shughuli mbalimbali za ardhi na kuzungumza na watumishi wa sekta hiyo katika halmashauri za wilaya ya Morogoro na Manispaa, ofisi ya kamishna wa ardhi mkoa na chuo cha ardhi.

Alisema ubabaishaji unaofanywa na baadhi ya maofisa ardhi umefanya wizara hiyo kuwa na doa mbele ya wadau mbalimbali wakiwamo wananchi, jambo ambalo uongozi wa wizara hautakubali uendelee ndiyo maana unatengeneza mfumo maalum kuondoa matatizo hayo.

"Dhuluma na malalamiko yanayotajwa kwa wananchi huwa ofisa ardhi hakosekani. Kama si wa kwanza, wa pili, watatu ndiyo maana tunaendelea kukumbushana hata kama hapa nyie hamhusiki," alisema Naibu Waziri.

Aliwaonya maofisa ardhi waliokwenda kufanya kazi katika wizara hiyo ili kupata ardhi, fedha au kwenda peponi, watambue kuwa hapo si eneo lao na kuwaonya juu ya mbinu chafu ambazo baadhi yao wamekuwa wakituhumiwa kuwafanyia wananchi wakiwamo wasio na uwezo wa kumiliki ardhi. "Kwingine mnachukua maeneo mazuri mnawaachia wananchi maeneo mabaya kwa sababu tayari mmefundishwa thamani ya ardhi au wanapotaka kupimiwa maeneo yao mnawaambia ni gharama kubwa kwa hiyo lazima asilimia kadhaa ya maeneo yanayopimwa yawe yao na asilimia nyingine ziwe kwenu na hapo hapo mnawalipisha tena fidia ya upimaji. Hii si sawa," alisisitiza.

Kutokana na tabia hiyo, aliwataka kuacha kuwa sehemu ya migogoro ya ardhi kwa kushindwa kusimamia na kutoa haki au kushauri kulingana na uhalisia wa mipaka. Aliwakumbusha kuwa jukumu la wizara ni kupima, kupanga na kumilikisha ardhi kwa maendeleo na si kutatua migogoro au kurasmisha ardhi ambako hufanyika baada ya matatizo.

Ridhiwani pia aliwahimiza maofisa hao pia kusimamia vizuri taaluma zao na mipango iliyopangwa ikiwamo matumizi bora ya ardhi na kulinda mipango miji ambayo inategemewa kwa maendeleo.

Pia alimwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ali Machela, kushirikiana na maofisa mipango miji kuwahamisha watu waliojenga milima ya Uluguru bila kibali, kwa sababu sheria ya ardhi iko wazi na haiwatambui watu hao. Alisisitiza kuwa watu hao wako katika maeneo hatarishi na yasiyoruhusiwa kwa mujibu wa sheria za mazingira.

# Fundi viatu ajenga daraja kuwasaidia wananchi kuvuka

**Na Owen Bariki,**
TUDARCo

FUNDI viatu, Azizi Masoud, ameamua kutumia ujuzi wake kutatua tatizo la wananchi kuvuka eneo moja kwenda lingine kwa kutengeneza daraja la mbao katika Mtaa wa Bondeni, Ubungo mkoani Dar es Salaam.

Kijana huyo ambaye hufanya kazi hiyo kila mara bila kuchoka, ameweka ndoo maalum ili mtu anapopita achangie chochote hali inayowezesha kupata wastani wa Sh. 5,000 kila siku.

Daraja hilo linaunganisha mtaa huo na mtaa wa Mawasiliano baada ya kuwapo ukosefu wa kivuko, hali inayosababisha wananchi kupata shida hasa wakati wa mvua kwa kushindwa kwenda kufanya shughuli za maendeleo.

Kutokana na kazi hiyo, wananchi wanaonufaika na huduma hiyo wameiomba serikali kuunga mkono kazi inayofanywa na kijana huyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, mmoja wa wananchi hao, Mathew Kagaruki, alisema kwa miaka minne Masoud amekuwa akitengeneza daraja la miti ambalo hudumu kwa muda mfupi, na bila msaada wowote licha ya kuwa jitihada zake huonekana kuzaa matunda kwa wakazi wa eneo hilo kwa kuwarahisishia kupita.

"Changamoto kubwa tunayokumbana nayo ni pindi maji yanapokuwa mengi na yakiwa yamechanganyika na uchafu. Watu hushindwa kabisa kupita kwenda mtaa mwingine, hivyo ujenzi wa kivuko hiki cha kudumu kitakuwa msaada mkubwa kwetu kwani kinachotengenezwa na Masoud kinaharibika haraka na kusababisha kurudia kujengwa mara kwa mara," alisema Kagaruki.

Omary Idi, mmoja wa wakazi wa eneo hilo, alibainisha kuwa viongozi wamekuwa wakiiona changamoto hiyo ya kivuko katika bonde hilo linalotenganisha maeneo hayo mawili, akidai kwamba wameifanya sehemu hiyo kama kigezo cha kuombea kura kipindi cha uchaguzi wakiahidi kupatengeneza watakapopewa nafasi.

"Kazi anayoifanya Azizi ni kubwa wawe na utu, watambue hata mchango wake maana kajitolea kufanya kazi kubwa kwa muda mrefu," alisema.

Kwa upande wake, Masoud alisema amekuwa akijitolea kwa kutumia ubunifu wake kutengeneza kivuko hicho kinachounganisha mitaa miwili, ikiwa ni moja ya msaada kwa wakazi wanaomzunguka.

Aidha, alitoa wito kwa serikali kuona umuhimu wa kutengeneza kivuko cha kudumu katika eneo hilo, ili kuwaondoshea wananchi kero hiyo.

"Awali watu walikuwa wanapita mtoni ndipo nilipoona haja ya kutumia ubunifu nilio nao kutengeneza daraja kwa kutumia miti ili wananchi wavuke upande wa pili. Naishukuru jamii kwa kutambua mchango wangu japo viongozi wanalifumbia macho kwani hakuna 'sapoti' yoyote," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Ubungo, Said Ramadhani, alisema wako katika hatua za mwisho za kutatua kero hiyo, huku akibainisha kwamba tayari kunafungu limetengwa japo hakutaja kiasi halisi, kinachotarajiwa kutumika kuanza ujenzi wa daraja hilo.

"Muda wowote daraja linatarajiwa kujengwa ili kuifungua njia na kuunganisha vijiji vyote viwili na litakuwa la kudumu kwa muda mrefu litakalowezesha watembea kwa miguu, bajaji na pikipiki kupita," alisema Ramadhani.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**IMEDURIWA - OMBI LA KUONYESHA NIA: KUBUNI NA KUTEKELEZA MIRADI YA UWEKEZAJI WA KIJAMII KWA MAKABILA YALIYO PEMBEZONI YANAYOJITAMBUA KAMA WAZAWA ASILIA. KUMBUKUMBU NAMBA. 10007446**

EACOP Ltd, Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi, inaalika taasisi (kampuni au AZAKI) zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kubuni na kutekeleza miradi ya uwekezaji wa kijamii kwa makabila yaliyo pembezoni yanayojitambua kama wazawa asilia yanayoguswa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) unatafuta huduma kutoka kwa shirika lenye uzoefu wa kutosha (Kampuni au AZAKI zinaweza kuitikia ombi la kuonyesha nia) ili kubuni na kutekeleza mipango ya uwekezaji wa kijamii na kujenga uwezo kwa jamii za makabila takribani thelathini (30) yaliyo Pembezoni yanayojitambua kama wazawa asilia yanayoguswa na Mradi wa EACOP Jamii hizi ziko katika mikoa ya Tabora, Manyara, Dodoma na Tanga.

Muundo wa programu utazingatia msaada kwa shughuli za kitamaduni (wafugaji au wawindaji) wa makundi haya ikijumuisha lakini sio tu usimamizi wa ardhi, afya ya mifugo na usimamizi, mahitaji maalum ya wanawake na inapaswa kuundwa kutumia mfumo wa pamoja unaozingatia mahitaji ya uhifadhi na uendelevu.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazooonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa uzoefu katika kubuni na kutekeleza miradi ya uwekezaji wa kijamii kwa makabila yaliyo pembezoni yanayojitambua kama wazawa asilia.
- Uthibitisho wa usajili na leseni ya sasa ya biashara kwa makampuni au usajili wa Asasi zisizo za kiserikali (AZAKI kwa Asasi zisizo za kiserikali (AZAKI).
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Ombi la usajili kwenye hifadhi data ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) na mrejesho wa wakat wa kuwasilisha nia unashauriwa sana kukusanywa.
- Kuzingatia kanuni za ushirikishaji wa wazawa za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya wazawa.
- Ubia kati ya makampuni/mashirika ya kitaifa na kimataifa unaruhusiwa.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi, uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usizidi **20Mb**) saa au kabla ya saa tisa kamili saa za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **24 August 2022.** Kichwa cha barua pepe kiwe **KUMBUKUMBU NAMBA. 10007446.**

Muhimu: Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi (kampuni au AZAKI) zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.

Taarifa zote za kuonyesha nia zinapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

216993202

# Waziri ataka kuondolewa urasimu biashara mipakani

**Na Mary Geofrey**

NAIBU Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, amesema Tanzania inaweza kupiga hatua kubwa zaidi kiuchumi, endapo mamlaka zinazosimamia biashara mipakani zitaondoa kodi ndogo ndogo na urasimu kwa wafanyabiashara. Pia amesema serikali itaendelea kupunguza vikwazo visivyo vya muhimu vinavyokwamisha biashara baina ya Tanzania na nchi jirani mipakani.

Kigahe aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizindua ripoti ya biashara za mipakani iliyofanywa na shirika lisilo la kiserikali la utafiti la Liberty Sparks.

"Kuwapo kwa kodi za kero na urasimu kunaharibu mfumo wa ufanyaji biashara na kuikosesha serikali mapato mengi," alisema Kigahe.

Alisema kutokana na changamoto hiyo, alisema serikali hukosa mapato kwa sababu wafanyabiashara hao hutumia njia za panya kufanya biashara zao.

"Rais Samia Suluhu Hassan yeye amesema ni kinara wa diplomasia. Unaposema ni kinara maana yake tunataka tushirikiane na wenzetu kwenye shughuli za kiuchumi. Hatuwezi kuwa na diplomasia ya uchumi bila kupunguza vikwazo kwenye mipaka," alisema Kigahe.

Alisema taasisi zinazosimamia mipakani kama vile Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), zinatakiwa kutoa elimu kwa wafanyabiashara wa mipakani ili kufuata taratibu za kufanya biashara na nchi jirani.

Kwa mujibu wa Kigahe, kutojengwa kwa wafanyabiashara hao ili kufahamu sheria na taratibu, Tanzania itaendelea kuwa soko la bidhaa kutoka nje ya nchi.

Pia alisema wataweka vivutio vya kikodi ili kuvutia wafanyabiashara kufanya biashara nchini na kukuza uchumi wa Taifa.

Naye Mkurugenzi wa Shirika hilo, Evans Exaud, alisema katika utafiti huo, wamebaini kuwapo kwa changamoto ambazo zikwamisha wafanyabiashara na biashara za mipakati na endapo yatabadilishwa serikali itapiga hatua kiuchumi.

Alisema kuna mifumo ya kielektroniki ya taasisi kutofanyakazi kwa pamoja, gharama kubwa za kodi na mlolongo wa upatikanaji wa vibali vya kufanyia biashara.

Alishauri mapendekezo hayo kufanyiwa kazi ili kuboresha biashara na kukuza uchumi wa wananchi na Tanzania kwa ujumla.




Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Hashim Komba (katikati), akikabidhi pikipiki kwa walimu wawili, baada ya uzinduzi wa mpango wa Benki ya NMB Mwalimu Spesho kwa wilaya hiyo, mkoani Lindi juzi. NMB itakuwa ikitoa mikopo ya pikipiki kwa walimu ili kuweza kuinua kipato chao katika mpango huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye hati za ardhi watakiwa kuwekeza

**Na Romana Mallya**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimewaita Watanzania wenye maeneo yaliyo na hati wanaoweza kushirikiana na kituo hicho kuanzisha uwekezaji wa aina mbalimbali wafanye hivyo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji TIC, John Mnali, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia mafanikio ya kituo hicho katika kipindi cha mwaka 2021/22 na mwelekeo wa vipaumbele vya bajeti 2022/23.

"Maeneo ya uwekezaji tunayohamasisha Watanzania walete ni yale yanayoweza kutumika katika sekta mbalimbali yawezekana eneo lako hati uliyokuwa nayo ni ya shamba, au ni ya kujenga hoteli, inawezekana hati uliyonayo ni eneo la makazi kwa maana kwamba eneo kubwa ambalo mwekezaji anaweza kujenga nyumba za kupangisha.

"Hata wale wenye leseni za madini, lakini uwezo wa mtaji haupo, TIC tunapokuwa na taarifa hizi zinatusaidia inapotokea mwekezaji anataka kushirikiana naye au kumuuzia inakuwa rahisi," alisema.

Pia, alihamasisha Watanzania kuchangamkia fursa za uwekezaji katika uzalishaji wa zao la parachichi ambalo soko lake ni kubwa.

Kuhusu mafanikio ya TIC, Mnali alisema katika kipindi cha Julai 2021 hadi Julai 2022, jumla ya miradi iliyosajiliwa na kituo hicho ni 274 ikilinganishwa na 234 iliyosajiliwa mwaka 2020/21 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 14.6.

"Miradi iliyosajiliwa katika kipindi hicho inatarajiwa kuzalisha ajira 43,925 ukilinganisha na ajira 36,470 zilizoripotiwa kipindi hicho mwaka 2020/21," alisema.

Alisema miradi hiyo ipo katika sekta ya viwanda, usafirishaji kilimo, ujenzi na majengo ya biashara, miundombinu ya kiuchumi, taasisi za fedha, rasilimali watu, usafirishaji, utalii na huduma.

Baadhi ya mradi uliosajiliwa 2021/22 aliutaja ni wa kampuni ya Taqa Arabia Tanzania ambao unatarajia kupunguza presha ya uingizaji wa bidhaa za petroli utakaojenga vituo 12 vya ubadilishaji wa magari binafsi, ya abiria na yale mazito kutoka kutumia petroli na dizeli na kutumia gesi.

Alisema utekelezaji wa vituo viwili vikubwa utakamilika robo ya mwisho ya mwaka huu na utatoa ajira za moja kwa moja 160, uwezo wake ni kilogramu 700,000 kwa mwaka za gesi. Aliutaja mradi mwingine wa uzalishaji wa sukari wa Mufindi Paper Mill ulioko Kasulu, mkoani Kigoma ambao unagharimu Dola za Marekani milioni 202 na utafanya uzalishaji wa miwa na usindikaji wa sukari kutoa ajira za moja kwa moja 9,000.

Mnali alitaja nchi ambazo zinafanya uwekezaji mkubwa Tanzania ni China, Marekani, Kenya, Uingereza, Mauritius, Afrika Kusini, Italia na Canada.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23 TIC imepanga kuendelea kuboresha mifumo ya kusajili ili kuongeza idadi ya miradi ya uwekezaji inayosajiliwa.

"Tutaboresha na kuimarisha huduma zitolewazo katika Kituo cha Huduma za Mahali Pamoja ili kufanikisha uwekezaji, kuendeleza mkakati wa kufuatilia na kutathmini miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa," alisema.

Pia alisema wanaendelea kutafuta ardhi kwa ajili ya uwekezaji, kuimarisha uwekezaji wa ndani na nje ya nchi kupitia makongamano na kufanya utafiti katika maeneo ya kuibua fursa, kuboresha mazingira na kuyaibua maeneo yenye fursa kwa ajili ya wajasiriamali wa kati na wadogo.

# Njombe sasa yapata mwekezaji parachichi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

ZIARA ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini Kenya Mei, mwaka jana, imezaa matunda baada ya mwekezaji wa kiwanda cha kuchakata parachini, AvoAfrica, kuja kuwekeza mkoani Njombe katika Halmashauri ya Mji wa Makambako.

Mkurugenzi wa kiwanda cha kuchakata parachichi, AvoAfrica, Nagib Karmali, alisema waliamua kuwekeza kwenye kiwanda hicho baada ya Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kufanya ziara nchini Kenya na kuwakaribisha kuwekeza nchini.

Alisema kiwanda hicho kinasafirisha tani 3,800 za parachichi kutoka Tanzania kwenda bara la Ulaya na Asia.

"Kiwanda hiki kina wafanyakazi zaidi ya 400 na pia tuna wakulima zaidi ya 2,200 ambao wanaleta matunda kiwandani," alisema Karmali.

Balozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Ali Jabir Mwadini, alisema wakulima wanatakiwa kuzalisha parachichi kwa wingi kwa kuwa bidhaa hiyo soko lake kubwa nchini Saudi Arabia.

Alisema hakuna sababu ya kuogopa ushindani wa kibiashara kwa kuwa kazi ya ubalozi ni kuunganisha wananchi na wazalishaji wa bidhaa katika masoko ya nje.

"Mimi naamini kwamba hakuna haja ya kuogopa ushindani kwasababu sisi bidhaa zetu hata tukizalishaje hatuwezi kujaza masoko, hii bidhaa yote ikienda Saudi Arabia inamalizika yote," alisema Mwadini.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, aliwataka wawekezaji wapya mkoani humo kuwasaidia kuwekeza pamoja na kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa.

Alisema serikali ya mkoa imejipanga kurahisisha uwekezaji ili kuwavutia wawekezaji.

"Sisi kama mkoa tutafanya vingi kwa niaba ya mwekezaji kama anahitaji kwenda TIC tutamsaidia, kama miundombinu ya maji tutamsaidia, umeme, barabara na hata kama unafuu wa kupata eneo halmashauri zetu zipo tayari," alisema Mtaka.

Alisema Halmashauri ya Mji wa Makambako ni eneo la kimkakati ambalo serikali ya mkoa inakwenda kuwekeza nguvu ili halmashauri hiyo iweze kuwa mstari wa mbele kiuwekezaji mkoani Njombe.

Pia alimwagiza mkurugenzi wa halmashauri hiyo kuweka kipaumbele upimaji maeneo ya uwekezaji ili kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza mkoani humo.

Aliwataka wananchi mkoani Njombe kulima kwa wingi miti ya matunda ya parachichi ili mwekezaji asihangaike kutafuta matunda hayo kutoka maeneo mengine.

Awali, Mbunge wa Jimbo la Makambako, Deo Sanga, aliishukuru serikali kuweka masharti nafuu kwa wawekezaji na kuwavutia kuwekeza hapa nchini.

"Ombi letu kubwa kwa balozi uwalete wawekezaji wengi ili waje kuwekeza katika mkoa wetu kwa kuwa parachichi nyingi hapa Tanzania zinatoka mkoa wa Njombe," alisema Sanga.

# Wajisaidia vichakani kwa kukosa vyoo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Igwamanoni, Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wanalazimika kujisaidia vichakani na nyuma ya madarasa wanayosomea baada ya vyoo walivyokuwa wakitumia kujaa na kutitia.

Shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 600 na matundu manne ya vyoo, mawili ya wanafunzi wa kike na mawili ya wanaume hali iliyowasukuma wazazi kujitoa na kuchimba matundu 12 ambayo yanasubiri ujenzi.

Diwani wa Bugarama, Prisca Musoma, alibainisha hayo katika kikoa cha Baraza la Madiwani cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2021/2022 kilichojadili masuala mbalimbali ya maendeleo na kumthibitisha Diwani wa Mwalugulu, Flora Sagasaga kuwa Makamu Mwenyekiti.

"Nilipopata taarifa ya kujaa na kutitia kwa vyoo nilifika shuleni hapo nikakutana na wanafunzi wanatoka kujisaidia vichakani, nilipozunguka nyuma vya vyumba vya madarasa nilikutana na vinyesi vya wanafunzi hali ambayo ilitia hofu sana," alisema Musoma.

Alisema, walimu ni watu wazima hawawezi kujisaidia vichakani kama wanafunzi wao, wanalazimika kutumia vyoo vya wakazi walipo jirani na shule hiyo na kuiomba halmashauri kukamilisha matundu ya vyoo 12 yanayoendelea kujengwa kwa nguvu za wazazi ili kutatua tatizo hilo.

Naye Diwani wa Ikinda, Matrida Musoma alisema, katika Shule za Msingi Ndililo, Balalogwa na Buzima matundu ya vyoo yaliyoko hayatoshelezi mahitaji ya wanafunzi na kila shule inawanafunzi zaidi ya 400 hali ambayo wakati wa mapumziko wanalazimika kuingia vyooni kwa awamu.

Pia, alisema wakati wa magulio na minada wafanyabiashara wanajisaidia vichakani na kwenye makazi ya watu kwa ukosefu wa vyoo huku halmashauri ikiendelea kukusanya mapato kupitia ushuru bila kujua athari zinazoweza kupatikana itakapotokea magonjwa ya mlipuko.

Alisema, ili kuondoa tatizo hilo ni vyema halmashauri ikafanya tathmini ya minada na magulio yasiyokuwa na vyoo na kujenga huduma hiyo kwa kuwa kuna baadhi ya minada ikiwamo wa Chakaya, ulitishiwa kufungwa na Ofisa Afya wa Kata baada ya wafanyabiashara kujisaidia ovyo.

Akijibu malalamiko hayo, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Charles Fussi, alikiri kupokea taarifa ya ukosefu wa vyoo katika shule hiyo kujaa na kutitia na kuahidi kuhakikisha analitatua tatizo hilo ili wanafunzi watakaporejea shuleni wakute miundombinu ya vyoo imaimarika vyema.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Msalala Iddi Kassimu Iddi alisema, akaunti za vijiji zina fedha nyingi na kila siku wanakaa vikao na kulipana posho na kumtaka mkurugenzi kuwaandikia barua wenyeviti wa vijiji na kuwaomba kutoa fedha za kujenga vyoo.

# Naibu waziri atoa siku 14 Bandari ya Karema ianze kazi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Uchukuzi, Atupele Mwakibete, ametoa wiki mbili kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kuhakikisha bandari mpya ya Karema inaanza kutoa huduma ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo na abiria kwa mikoa inayozunguka Ziwa Tanganyika na nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Akizungumza baada ya kukagua mradi huo mkoani humo ambao umekamilika kwa asilimia 100, Naibu Waziri Mwakibete alisema kukamilika na kutoa huduma kwa bandari hiyo iliyogharamiwa na serikali kwa fedha za ndani zaidi ya Sh. bilioni 30 kutachochea uchumi wa mkoa na nchi kwa ujumla.

"Fedha nyingi zilizowekwa hapa lazima zianze kutumika vitu vilivyobaki ni vichache sana na viko ndani ya uwezo wetu hivyo tuvikamilishe haraka na tuanze kutoa huduma muda hausubiri na mradi umeshakamilika," alisisitiza Naibu Waziri Mwakibete.

Alisema pamoja na mradi huo serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23 inaendelea na ukarabati wa meli ya MT. Sangara na imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya mbili za abiria na mizigo zitakazotoa huduma katika bandari za Ziwa Tanganyika na nchi za jirani.

Mwakibete aliwataka TPA kuhakikisha wananchi wa Kata ya Karema wanapewa kipaumbele cha ajira hususani kwa kazi zisizohitaji utaalamu sababu ajira hizo zitachochea uchumi wao pia walinzi wa miundombinu hiyo ili iweze kudumu.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Onesmo Buswelu, aliwataka wananchi kuunda vikundi vidogo ili kutumia fursa ya uwapo wa mradi huo mkubwa kupata ajira za muda mfupi na mrefu wakati itakapoanza kufanya kazi.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Edward Mabula, alisema mradi kwa sasa umeshakamilika na kumhakikishia Naibu Waziri kuwa kazi zilizobaki ni kufunga umeme itakayofanyika kwa wiki moja pamoja na uletaji wa mitambo ya kuhudumia mizigo.

"Huduma hapa itaanza wakati wowote sababu baada ya kuunganisha umeme, tutafanya majaribio kwa siku chache na baadaye tutakamilisha taratibu za uendeshaji na tutaanza kutoa huduma," alisema Kaimu Meneja Edward Mabula.

Naibu Waziri yuko mkoani Katavi kwa ziara ya siku mbili ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.



Kaimu Meneja wa Bandari ya Ziwa Tanganyika, Edward Mabula, akimwonesha Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, baadhi ya miundombinu ya bandari iliyokamilika, alipotembelea mradi wa ujenzi wa Bandari ya Karema mkoani Katavi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hospitali Bombo yapata maabara kupima UVIKO-19

**Na Yasmine Protace**

MAABARA mpya ya upimaji wa sampuli za UVIKO-19 katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Bombo, Tanga itarahisisha upatikanaji wa huduma kwa haraka zaidi na kuwapunguzia wananchi adha ya kusubiri majibu kwa muda mrefu.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu kwenye hafla ya uzinduzi wa maabara ya upimaji wa sampuli za UVIKO-19 iliyofanyika katika Hospitali ya Rufani Bombo, iliyohudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Maendeleo na Ushirikiano wa Uchumi kutoka Serikali ya Ujerumani, Dk. Bärbel Kofler.

"Tumefungua kituo hiki cha kupima sampuli za UVIKO-19 kwa kutumia kipimo hiki cha PCR, sasa hivi kikianza kufanya kazi hapa Bombo mtu akipima UVIKO-19 majibu yanaweza kutoka mapema ndani ya saa nane," alisema.

Alisema, awali sampuli za vipimo za UVIKO-19 zilikuwa zinatumwa kwenda Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii jijini Dar es Salaam na kuchukua muda mrefu wananchi kusubiri majibu.

Waziri Ummy alisema, ujenzi umegharimu Sh. milioni 225 huku ikiwa ni maabara ya 11 nchini yenye uwezo wa kufanya vipimo hivyo vya UVIKO-19.

Pia, ameishukuru Serikali ya Ujerumani kwa kuendelea kusaidia sekta ya afya nchini kupitia Programu ya Tumaini la Mama ambayo imelenga kuboreshaji utoaji wa huduma bora za afya kwa kutoa bima za afya kwa wajawazito na watoto wao (wasio na uwezo)

Kwa Upande wake Dk. Kofler alisema, wanaamini kituo hicho sasa kinakwenda kutoa huduma za vipimo kwa wakazi wa Tanga na maeneo jirani ya hapo. Kuna umuhimu mkubwa sana kwetu sisi Ujerumani kushirikiana na mataifa mengine katika mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Dk. Kofler alisema kuwa Serikali ya Ujerumani inaendelea na mpango wa kusaidia nchi nyingine ulimwenguni kupata chanjo dhidi ya UVIKO-19 na wamejipanga kutoa dozi zaidi ya bilioni 7.2 za chanjo.

Aidha, alipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutoa hamasa na elimu ya chanjo dhidi ya UVIKO-19 na kuahidi kuwa Serikali ya Ujerumani itaendelea kushirikiana na Tanzania katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo pamoja na mambo mengine.

# Ujenzi holela wakwamisha kasi miradi ya barabara

**Na Beatrice Moses**

KASI ya miradi ya ujenzi wa barabara katika baadhi ya maeneo jijini Dar es Salaam, imeelezwa kukwamishwa na ujenzi holela wa nyumba.

Nyumba nyingi zinadaiwa kujengwa maeneo ambayo inapita miundombinu hiyo ya barabara, hasa Wilaya ya Ubungo na kusababisha wakazi wake kuendelea kupata kero hasa wakati wa mvua.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Heri James, ameyasema hayo wakati akizunguza na Nipashe kuhusu miradi kadhaa ya barabara na madaraja inayotekelezwa katika wilaya hiyo na kubainisha kuwa kuna miradi kadhaa ya barabara inachelewa kuanza kwa sababu nyumba zimejengwa kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi ya barabara.

Alisema, changamoto iliyopo ni fedha iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi haitoshi kulipa fidia ya kuwahamisha waliojenga kwenye eneo lililotengwa kupita barabara.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Ubungo, Mhandisi Musa Mzimbiri, ametaja baadhi ya miradi iliyokwama kuanza kuwa ni wa barabara ya urefu wa kilomita 9.5 ya Suka kupitia Saranga hadi Kinyerezi ambayo inapaswa kuwa na upana wa mita 12 na baadhi ya maeneo ina upana wa mita tisa.

Mhandisi Mzimbiri alisema Sh. milioni 500 zimetolewa ili kuanza mradi wa ujenzi wa barabara ya zege unaotajwa kuwa ni muhimu kwa kuwa unaunganisha wilaya za Ubungo na Ilala.

Mradi mwingine ni wa King'ong'o Msakuzi hadi Kimara Mwisho wenye urefu wa kilomita moja, ambao unapaswa kujengwa kwa kiwango cha zege, lakini umekwama kuanza na mazungumzo yanaendelea ili kupata ufumbuzi.

Maeneo kadhaa katika Wilaya ya Ubungo yana udongo wa mfinyanzi ambao wakati wa mvua husababisha utelezi na kuwa kero kwa watumiaji wa barabara hizo.




Mkurugenzi Mkuu wa Pesapal Tanzania, Bupe Mwakalundwa (katikati), akipokea leseni iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kwa ajili ya kufanya biashara ya kutoa huduma kwa mifumo ya malipo ya kidijitali kutoka kwa Meneja Msimamizi wa Wateja wa kampuni hiyo, Ally Abdu, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Mauzo Pesapal Tanzania, Everline Simpilu. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Waelezwa umuhimu kupima afya kwa fursa za ajira

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

NAIBU Waziri wa Habari Teknolojia ya Mawasiliano na Habari, Mhandisi Kundo Mathew amewataka wananchi kujenga tabia ya kupima afya ili kujilinda na magonjwa, na kupata fursa ya ajira.

Alitoa rai hiyo juzi alipokuwa akizungumza kwenye shughuli ya upimaji wa afya ya mama na mtoto iliyoandaliwa na Tanzania Women Advocate Journalist for Children Rights (TAWOJAC), iliyofanyika Mailimoja, Kibaha.

Alisema, kitu kilichofanywa na waandishi hao ni kujenga uelewa kwa Watanzania wazingatie umuhimu wa kupima afya zao na baadaye wajue hali zao na hatua za kuchukua.

"Bila kuwa na nguvu kazi uchumi wetu hauwezi kuimarika na bila kuwa na afya nzuri hata miradi inayokuja tutajikuta tunaingiza watu wengine kutoka nje ya nchi waje kufanya kazi kwasababu utakuta sisi afya zetu haziturusu kwenda kufanya kazi hizo."

"Ni vizuri tukapima afya mara kwa mara kwasababu Watanzania wote ni nguvu kazi ya kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan, anafanya jitihada ya kuleta miradi mingi, isikosekane nguvu ya kutekeleza hiyo miradi," alisisitiza Mhandisi Kundo.

Kadhalika, alitoa wito kwa TAWOJAC, kufanya utaratibu huo kuwa endelevu katika maeneo mengine nchini ili wananchi wote wapate fursa ya kupima afya zao.

Mkurugenzi wa TAWOJAC, Neema Pius, alisema Taasisi hiyo ya kutetea haki ya mama na mtoto imeandaa upimaji huo baada ya utafiti walioufanywa na kubaini kuwa wapo wanawake wanashindwa kwenda kupima afya zao kutokana na gharama kwenye maeneo yanayotoa huduma za afya . "Tulifanya utafiti mdogo kuwahoji kinamama namna gani wanapata matibabu, wengi wao wakatuambia kwamba, huwa hawaendi kupata hospitalini kwasababu gharama ni kubwa, hivyo anaamua kumeza panadol, tukaamua kubuni wazo hili kwamba tuna uwezo wa kufanya zoezi hili kupitia mwanamke akajua afya yake," alisema.

Alisema, lengo la upimaji huo ni kuamsha ari kwa mwanamke na mtoto ili awe na tabia ya kupima afya yake mara kwa mara kuliko kungoja magonjwa ya ghafla ambayo yanaweza yakampata ambayo matibabu yake ni makubwa.

Alisema, upimaji huo utakuwa endelevu na kwasasa wameanza na mkoa wa Pwani, katika Wilaya ya Kibaha wataendelea katika wilaya nyingine kila baada ya miezi mitatu.

Mkurugenzi huyo, alimshukuru Mkuu wa Majeshi ambaye aliridhia Taasisi hiyo na kutoa madaktari wake na vifaa bure kwa ajili ya shughuli hiyo ya upimaji, alishukuru pia ushirikiano wa Mkuu wa Wilaya ya Kibaha na Rais wa Chama cha Madaktari wa Watoto Tanzania.

Akizungumzia upimaji huo, Mkuu wa kikundi cha upimaji kutoka Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Luteni Kanal Tumenye Mwalukunga, alisema walifanya upimaji wa malaria kwa watoto, uchunguzi wa saratani ya matiti na upimaji wa presha.

Alisema, waliobainika kuwa na viashiria vya saratani ya matiti watapelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi kwa ajili ya matibabu.

Sophia Mohamed, Mwanaisha Said na Mwaus Ally ni kati ya waliojitokeza kwenye upimaji huo na kuishukuru Taasisi ya TAWOJAC kwa kuwafikishia huduma hiyo kutokana na wanawake kuwa na magonjwa mengi yanayowasumbua na kukosa fedha za kwenda kufanyiwa upimaji.

Wameomba taasisi nyingine na mashirika kuwafikishia huduma hiyo mara kwa mara ili wapime afya zao bure.

## Waziri Mkenda mgeni rasmi mahafali waliosoma nje

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya tatu ya wanafunzi waliosoma vyuo vikuu nje ya nchi yanayotarajiwa kufanyika mwishoni mwa wiki.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Wakala wa Vyuo Vikuu nje ya nchi, Global Education Link (GEL), Abdlulmalik Mollel, alisema hayo wakati akizungumzia mahafali hayo.

Alisema, mahafali hayo ni ya wanafunzi waliobahatika kusoma nje ya nchi na kuhitimu, yatakayofanyika Mlimani City, jijini Dar es Salaam.

Alisema mabalozi wa nchi mbalimbali ambazo vijana hao wamesoma wamethibitisha kushiriki katika mahafali hayo.

"Ili mahafali haya yafane, mlengwa mkubwa ni mzazi na mtoto wake kwasababu mwanafunzi aliyesoma nje anakuja kusherehekea na wazazi na walezi waliojinyima kumlipia ada hivyo wanafunzi wamethibitisha kushiriki," alisema.

Mollel alisema wanafunzi wanaotarajia kwenda nje ya nchi kusoma wataalikwa ili waweze kujifunza kutimiza malengo yao kama wenzao walioenda kusoma wakahitimu na wakarudi nyumbani kuleta ujuzi kusaidia maendeleo ya nchi yao.

Alisema wanafunzi wa kitanzania watakaokwenda nje ya nchi watabebeshwa malengo ya kuitangaza nchi ili kusaidia jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye anaitangaza nchi kwenye maeneo mbalimbali duniani.

"Tunamwona mama yetu anavyokwenda nje ya nchi yetu kuisemea katika rasilimali tulizonazo, fursa na uzuri wa nchi yetu sasa peke yake hataweza tunataka Watanzania watakaokwenda nje sasa hivi kuitangaza nchi liwe ajenda ya kipaumbele," alisema Mollel.

Alisema anataka kuona mwanafunzi anayekwenda nje ya nchi anarudi na wawekezaji kwenye nyanja mbalimbali kama elimu na utalii badala ya kuhitimu na kurejea nchini wakiwa na vyeti vitupu.

Alisema kuhitimu au kushindwa kuhitimu nje ya nchi kunategemea uwajibikaji wa mwanafunzi anapokuwa nje ya nchi hana usimamizi wa wazazi na walezi au taarifa potofu walizopata kuhusu vyuo wanavyoenda kusoma.

Mollel alisema kuna wanafunzi wanaenda kusoma nje ya nchi kwa kuchagua vyuo kwenye mitandao na wanapogundua kwamba havitambuliki wanaamua kuahirisha masomo.

"Kuna changamoto ya ada, mwanafunzi anasoma chuo ambacho kinalazimisha ada ilipwe yote kwa wakati mmoja na mzazi anakwama kulipa na anazuiwa kuendelea, lakini kupitia GEL lazima ahitimu kwanza mambo mengine yafanyike baadaye," alisema.

Alisema kuna mambo mengi yanayosababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kuhitimu nje ya nchi ikiwamo kujiingiza kwenye mambo yasiyohusiana na masomo kutokana na kukosa usimamizi sahihi anapokuwa anaendelea na masomo.

Alisema mahafali hayo ni daraja kwa wanafunzi hao kukutana na wawekezaji mbalimbali ili kama kuna fursa za ajira waweze kuchukua vijana hao ambao alisema wamehitimu kwa ufaulu mzuri.

ama
ALHAMISI AGOSTI 18, 2022
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

**Msalaba Mwekundu unavyojitosa kulisha watoto, kukabili utapiamlo**



Ukurasa 13

MJUMITA, FAO kugeuza vijiji 'majangwa' kuwa misitu minene



Ukurasa 14


**Tambua misitu ilivyo moyo wa nishati mijini na vijijini**

AFYA

# Mapele ngozi maradhi yanayotishia uchumi, afya mifugo na wafugaji

• Chanjo yake pasua kichwa ni 280,000/-

**Na Jumbe Ismailly,** HANANG



Ugonjwa wa mapele katika ngozi licha ya kuua mifugo kwa wingi, chanjo yake ni ya gharama kubwa. **PICHA: MAKTABA**

KAMA ilivyo kwa binadamu, wanyama nao wana maradhi ambayo wakati mwingine huwaambukiza watu kadhalika, hudhibitiwa kwa chanjo na tiba nyingine.

Wanyama wanashambuliwa na maradhi ya ngozi kama yanavyomtesa binadamu na kwa upande wa mifugo upo ugonjwa wa 'mapele ngozi' unaoshambulia ng'ombe wakati wa umri wowote na kusababisha hasara kiuchumi kutokana na kuharibu ngozi yote ya mifugo.

Maradhi hayo huenezwa na virusi viitwavyo Lumpy Skin Disease Virus na kwa mara ya kwanza mwaka 1929 ulitambuliwa nchini Zambia, baadaye Botswana, Zimbabwe na Afrika Kusini.

Ilipofika 1957 uliripotiwa Kenya na huenda ndiyo wakati ulifika Tanzania kutokana na wafugaji wa mataifa hayo kuchangia malisho wakivuka mipaka kusaka maji na nyasi.

Mapele ngozi yanawaambukiza wanyama kwenye mikoa mbalimbali tena ni rahisi kuyabaini kwa sababu ya kushambulia na kubadilisha ngozi ya mifugo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Hanang, mkoani Manyara, Elizabeth Lusingu, anazungumzia jinsi ya kukabiliana na maradhi hayo akisema, ni pamoja na kuwahimiza wafugaji kuchanja wanyama wao ndiyo njia muhimu ya kupunguza hata kumaliza mashambulizi dhidi ya mifugo.

Hanang ina ng'ombe 282,111 inatumia njia mbalimbali kukabiliana na magonjwa ya ngozi ya mifugo ikiwamo kuichanja na majosho kuiogesha, anasema.

Chanjo ya ugonjwa wa mapele ya ngozi hutolewa Juni, Julai, Agusti, Septemba, Oktoba na Novemba na kwamba, kuanzia mwaka 2019 huku 2021 ng'ombe 4,924 walichanjwa kuzuia maradhi hayo, anaongeza.

"Mwaka 2019 ng'ombe 2, 278 walichanjwa huku 2020 walichanjwa 2,646 na mwaka jana hakuna aliyepatiwa kinga ya ugonjwa huu," anafafanua Mkurugenzi Elizabeth.

Hanang' ilijiwekea lengo la kuchanja ng'ombe 389,746 kuanzia mwaka 2019 hadi 2021, lakini malengo hayo hayakutimia kutokana na sababu mbalimbali.

Mkurugenzi anazitaja baadhi ya sababu kuwa ni pamoja na wafugaji kuhamisha mifugo yao wakati wa chanjo na kukosa mwamko wa huduma za chanjo, linalohitaji kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa wafugaji hao.

Anaongeza kuwa, mwitikio wa wafugaji wakati wa chanjo bado ni mdogo kutokana na baadhi kutaka wanyama wachanjwe bure wasigharamiwe huku wengine wanapopata taarifa za chanjo wanahamisha mifugo yao.

"Kutokana na kuhamisha mifugo wamesababisha kukwamisha malengo. Na pia uhaba wa vitendea kazi kwa wataalamu wakati wa kupeleka chanjo vijijini kumetukwamisha na wakati mwingine njia nyingine kutopitika wakati wa masika na ukosefu wa fedha," anasema Elizabeth na kutaja vitendeakazi vya wataalamu hao kuwa ni magari, pikipiki, vifaa vya kubebea chanjo ili isiharibike.

Akizungumza kwa niaba ya wafugaji wa wilaya hiyo, mfugaji Emmanuel Moleli, anaishauri kuweka ruzuku kwenye dawa za chanjo kama ilivyofanya kwenye pembejeo za kilimo ili iwe njia rahisi kwa mfugaji kupata huduma za chanjo

Moleli anayeishi katika Kijiji cha Balang'idalalu anazitaja changamoto walizonazo wanapohitaji chanjo hiyo kuwa ni pamoja na ukubwa wa gharama za chanjo na kutoa mfano kuwa chanjo ya ugonjwa wa miguu na midomo (FMD) kuwa ni Shilingi 280,000 kwa ng'ombe moja.

Changamoto nyingine ni wafugaji kukosa mwamko wa kuchanja na idadi kubwa ya wafugaji kupuuza kuchanja hata kuku, kwa madai kuwa hakuna faida.

Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Hanang, Kenneth Ngadada, anasisitiza kwamba iwapo ng'ombe hawatachanjwa kuwakinga mapele ngozi, wafugaji hawatakwepa madhara kama kupoteza wanyama wengi kwa wakati mmoja maradhi yakizuka.

Madhara mengine ni kukosa kipato kutokana na vifo vya mifugo pia kusambaza maradhi kutoka sehemu moja kwenda nyingine pamoja na masoko ya nje ya mifugo kupata nyama zenye maradhi.

Aidha, Ngadada anasisitiza kwamba pamoja na wilaya hiyo kuandaa ratiba ya kutoa chanjo za mifugo kwa mwaka mzima haitekelezeki kutokana na uhaba wa fedha miongoni mwa wakulima.

Ofisa Mifugo na Uvuvi anazitaja kata ambazo wafugaji wake hawakupeleka mifugo yao kupatiwa chanjo kuwa ni Bassodesh, Bassotu, Garawja, Getanuwas, Masakta, Balang'idalalu, Gidahababieg, Gisambalang', Sirop, Endagaw, Endasak, Ishponga, Laghanga, Mulbadaw na Dawar.

Halmashauri hiyo inaendelea na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa chanjo kwa mifugo na kwa wafugaji wa wilaya hiyo, anaongeza ofisa huyo.

Ngadada akizungumzia sheria za kudhibiti magonjwa ya mifugo, zinavyoelekeza kwa wasiotekeleza maagizo ya chanjo Sheria namba 17 ya 2003 inaelekeza kuwa yeyote asiyechanja adhabu yake ni kulipa faini kuanzia Shilingi 300,000 na isiyozidi

**INAENDELEA UK.12**

MAZINGIRA

BALAA UNAPOTIKISA

# Msalaba Mwekundu unavyojitosa kulisha watoto, kukabili utapiamlo



Mazingira ya ukame kama haya yanasababisha mifugo kufa kwa njaa na hata watoto kukumbwa na utapiamlo.

**Na Yasmine Protace**

UKAME wa muda mrefu umekuwa gumzo kwa baadhi ya wilaya za mikoa ya Arusha na Manyara huku ukisababisha familia za wafugaji kukosa chakula, wagonjwa na watoto wadogo wakidhoofu na wengine kupata utapiamlo.

Kutokana na mazingira hayo, Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS), kimeweka kambi kusaidia familia hizo ikiwa ni pamoja na kuwapatia msaada wa vyakula na vitu mbalimbali kuimarisha afya zao hasa ungalishe, matunda na fedha taslimu.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Rais wa TRCS, David Kihenzile, anasema wamezifikia kaya 1,200 na kuzipa msaada huo akiongeza: "Tulifika huko na kupokelewa na mwenyeji wetu Fredrick Lowassa ambaye ni Mbunge wa Monduli kuelekea Kijiji cha Idonyonaado ambacho ni mojawapo ya vijiji vilivyoathiriwa na ukame na kuwapa misaada vilevile tukatoa Sh.210,000 kwa kaya 114 za kijiji hicho," anasema Kihenzile.

> **Hatuishii hapo pia chama kinasaidiana na Wizara ya Afya kutoa elimu kwa jamii na kufuatilia kujua ni jinsi gani jamii inavyozungumzia corona.**

Rais huyo anaongeza kuwa, pamoja na msaada huo wa pesa, wamejikita zaidi katika kutoa misaada ya kibinadamu ili kurejesha afya za waathirika wa ukame na kuweka salama dhidi ya maradhi yanayosababishwa na janga hilo la njaa.

"Mwezi uliopita tumetoa Shilingi milioni 216 kwa kaya 1,200 katika mikoa ya Arusha na Manyara ikiwa ni mwendelezo wa chama chetu kusaidia familia zilizoathiriwa na ukame," anasema.

Rais huyo anasema, Februari mwaka huu walianza kutoa huduma hizo za fedha na vyakula kwa kaya 700 katika wilaya za Longido mkoani Arusha, Simanjiro na Mbulu mkoani Manyara ambapo kila kaya ilipata Sh.140,000.

"Kaya nyingine 150 ziligawiwa ungalishe, matunda, dawa na kufundishwa jinsi ya kupika uji huo kwa ajili ya watoto. Tutaendelea kuwa na jamii hiyo wakati wa maafa na wananchi waendelee kuwa na imani nasi," anasema Rais wa TRCS.

Anafafanua kuwa, wanafanya juhudi hizo ili watoto wasikumbwe na utapiamlo kwa kuwapa ungalishe na kuwafundisha wazazi na walezi kuupika na kuwalisha watoto kwa lengo la kuboresha afya zinazotishiwa na njaa.

Katika ufafanuzi wake, anasema chama hicho kinafanya kazi ya kuhudumia jamii, kwa uwezeshwaji wa Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Msalaba Mwekundu (IFRC), ili kuwafikia wafugaji hao na kuwaweka watoto wao kwenye salama kiafya.

"Hatuishii hapo pia chama kinasaidiana na Wizara ya Afya kutoa elimu kwa jamii na kufuatilia kujua ni jinsi gani jamii inavyozungumzia corona," anasema.

**WITO KWA WALENGWA**

Mbunge wa Monduli, Fredrick Lowassa, ambaye moja ya vijiji vya jimbo lake vimekumbwa na ukame kikiwamo cha Idonyonaado, anatoa wito kwa walionufaika na msaada kutumia kwa kile kilichokusudiwa.

"Kwanza niwashukuru Msalaba Mwekundu, lakini niwaombe wananchi kutumia fedha kununua mahitaji muhimu kikiwamo chakula na siyo mambo mengine," anasema Lowassa.

Anaongeza kuwa miundombinu ya barabara ya Idonyonaado ni mibovu na kwamba chama hicho kimefika eneo hilo bila kujali hali hiyo, hivyo hana budi kuwashukuru kwa uamuzi huo wa kuwasaidia wananchi wake.

Kaimu Ofisa Maafa wa Wilaya ya Longido, Albert Israel, ambaye msaada huo umefikishwa katika eneo lake, anawataka waliopata kuutumia kuhudumia familia zao.

"Inawezekana mkadhani msaada huu unaweza kuwa unatolewa kwenu tu, lakini kumbukeni kuwa Tanzania ni kubwa, chama hiki kinahudumia maeneo mengi ya nchi, hivyo, msaada utumike ulivyokusudiwa," anasema Israel. Meneja Maafa wa chama hicho Samuel Katamba, anabainisha kuwa kinatoa huduma mbalimbali katika jamii pale majanga yanapotokea yakiwamo yanayosababishwa na vita, magonjwa na mambo mengine.

"Tunachohitaji ni ushirikiano wenu tunapotimiza majukumu yetu kwenu hasa wakati wa majanga yakiwamo ya asili kama ukame, hivyo tupo pamoja katika shida na raha tuendelee kushirikiana," anasema Katamba.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Idonyonaado, kwa jina moja la Leah anasema, ukame unachangia watoto wao waugue kutokana na kukosa lishe, huku mifugo ikikosa maji na nyasi na kufa.

Tunashukuru Msalaba Mwekundu kwa jitihada mnazofanya za kutusaidia kwa hali na mali ili kukoa maisha yetu na mifugo yetu, ninawaombea kwa Mungu mwendelee na moyo huo," anasema Leah.

## Mapele ngozi maradhi yanayotishia uchumi, afya mifugo na wafugaji

**INATOKA UK.11**

500,000 au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.

**MAGONJWA MENGINE**

Ngadada anataja magonjwa yanayosumbua mifugo katika wilaya hiyo kuwa ni homa ya malale (trypanosomiasis), ndigana baridi (anaplasimosis), kukojoa damu (babesiosis), homa ya mapafu (CBPP), chambavu, sotoka ya mbuzi na kondoo (PPR), na ndigana kali (ECF).

Anasema, ili kupambana na maradhi hayo wilaya hiyo ina kalenda ya kutoa chanjo ya mifugo kila mwaka ili kukinga magonjwa ambukizi.

Akizungumzia changamoto walizokumbana nazo wakati wa kuchanja Ngadada, anasema wafugaji wengi kutopeleka mifugo kwenye chanjo, uhaba wa usafiri kwa wataalamu kwenda vijijini kuchanja mifugo pamoja na baadhi ya njia kutopitika msimu wa masika.

Anatoa wito kwa wafugaji wanapopata taarifa ya chanjo kupeleka mifugo yao kwenye chanjo na kuwataka maofisa ugani kuwaelimisha wafugaji umuhimu wa chanjo za mifugo na pia kuwakumbusha wanasiasa kuhamasisha wafugaji kuchanja mifugo.

Bariki Shayo ni mmiliki wa duka la dawa za mifugo katika Mji wa Hanang anasema, upatikanaji wa dawa katika halmashauri hiyo ni rahisi kwani kuna maduka ya pembejeo yanayouza chanjo mbalimbali za mifugo.

Anasema Shayo, ambaye ni mtaalamu wa mifugo katika Halmashauri ya Hanang kwamba kwa kiasi kikubwa serikali imejitoa katika shughuli za kutoa chanjo na kwa mara ya mwisho ilitoa chanjo kwa wafugaji mwaka 2012.

Wilaya ya Hanang, mkoa wa Manyara una jumla ya ng'ombe 282,111, mbuzi 192,300, kondoo 102,751, punda 17,501,nguruwe 10,019, mbwa 17,501, paka 9,927, sungura 9,641, kuku 279,922, bata 155,797 na kanga ni 1,078 hivyo kufanya mifugo yote kufikia 1,078,064.

MAZINGIRA

# MJUMITA, FAO wako Kilosa kugeuza vijiji 'majangwa' kuwa misitu minene

## • Shule, kanisa, misikiti wamo kupanda miti

Na Beatrice Philemon

UNAPOZUNGUMZIA athari za mabadiliko ya tabianchi si Watanzania wengi wanaofahamu dhana hiyo na hatari zake, licha ya kwamba wameona mabadiliko kama kuwapo jua na joto kali, mafuriko, vimbunga, ukame, baridi kali na upepo mara kwa mara.

Wadau na washirika mbalimbali wameanza kampeni za kuelimisha jamii na pia kuchukua hatua kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, mojawapo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro.

Ikishirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), imeanzisha mradi wa upandaji miti unaojulikana kama " Mradi wa Misitu na Kilimo".

Ofisa Mradi wa MJUMITA, Hamisi Masinde, anazungumza na Nipashe, akisema ni mradi wa mwaka mmoja unaolenga kuboresha uoto wa asili, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kubadilisha maisha ya jamii.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Majid Mwanga, ndiye anayeuzindua katika Shule ya Msingi Ulaya-Mbuyuni na unawashirikisha wanavijiji vya Ulaya-Mbuyuni, Unone, Mbamba na Ihombwe katika halmashauri hiyo ya Kilosa.

Kazi hiyo inafadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO), anasema Masinde, na kuongeza kuwa hadi sasa mradi umewafunza wananchi na wanafunzi kuanzisha vitalu vya miti, kupanda miti kwenye maeneo yao na kuisimamia kikamilifu.

Kupitia mafunzo hayo, miche 33,807 imeoteshwa na mingine imepandwa kwenye taasisi zilizoko kwenye Kata ya Ulaya-Mbuyuni na baadhi ya kaya za Kijiji cha Ihombwe na Ulaya-Mbuyuni, anasema Masinde.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji Ulaya-Mbuyuni, Titima Mohamed, anasema wanafunzi wa Ulaya Mbuyuni wamejifunza jinsi ya kuotesha miche ya miti na sasa ni wadau wazuri wa kuhifadhi mazingira.

"Kabla ya kupata mafunzo, tulianza kufanya tathmini ya mabadiliko ya tabianchi na jinsi wanajamii wanavyohimili," anasema Mohamed.

Baada ya tathmini hiyo, ilibainika kuwa kuna uhitaji wa kuanzisha vitalu vya miti katika vijiji vya wilaya hiyo ili kupunguza utegemezi mazao ya misitu usiokuwa wa lazima lakini unaochangia kuharibu mazingira na misitu ya asili, anaongeza.

Novemba mwaka 2021, Kijiji cha Ulaya Mbuyuni kilianza kutekeleza mradi wa upandaji miti kwa lengo la kuzalisha miche 50,000, anaeleza.

"Lengo kuu la mradi ni kuboresha na kutunza mazingira yetu kwa kupanda miti na kuhifadhi misitu ya vijiji, kuwashawishi wanakijiji waone umuhimu wa kupanda miti na kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi," anasema Mohamed.

Wameotesha miti aina mbalimbali ikiwamo miche 9,600 misederela, 4,200 mitiki, wakati mikongo ni 4,007 na 1,000 ni mikangazi jumla yote ni miche 15,000, anasema Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji.

"Mradi wa upandaji miti Ulaya-Mbuyuni ni endelevu, hivyo basi, tunaomba kama kuna fursa za wadau mbalimbali wanaosaidia katika mradi wa uzalishaji wa miche ya miti tunaomba watuunge mkono kwenye jukumu hili," anasema.

Mbali na hilo, kupitia mradi wa misitu na kilimo, Halmashauri ya Kilosa kwa kushirikiana na MJUMITA, wamefanya shughuli mbalimbali kama vile kuanzisha vikundi vya biashara ya samani na ujenzi wa nyumba (kupaua) kwa vijana kuanzia miaka 18-30 wa vijiji vya Unone na Ihombwe.

Halikadhalika, kuandaa mpango wa biashara ya mkaa, kuanzisha na kuvijengea uwezo vikundi vya hisa kwa vijana kutoka vijiji vya Ihombwe, Mbamba na Unone.

Pia, anasema wametoa mafunzo ya utawala bora, jinsia na usimamizi wa fedha kwa viongozi wa vikundi vya uzalishaji wa mkaa kutoka vijiji vya Mbamba, Msimba, Ulaya-Mbuyuni, Ihombwe, Kitunduweta na Rudewa Gongoni.

Anasema Kijiji cha Ulaya Mbuyuni kilichoanza mwaka 1976, kina wakazi 3,257, kati ya hao wanawake 1,640, wanaume 1,617.

Anaeleza kuwa, Ulaya Mbuyuni ni miongoni wa vijiji vinavyotekeleza Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu Tanzania na tayari wametenga msitu wenye ukubwa wa hekta 3,540 na kutangazwa kwenye gazeti la serikali na kupewa namba GN namba 688.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mjumbe wa Bodi ya MJUMITA, Juliana Mwenda, anasema mradi huu umelenga shule za msingi, sekondari, taasisi za serikali pamoja na za kidini ikiwamo makanisa na misikiti.

"Tumeanza kusambaza miche ya miti shuleni kwa sababu ndiyo kizazi kinachokuja na kinachokua, kikianza kupata uelewa wa kupanda na kuhifadhi tunaamini hapo baadae taifa litanufaika na misitu na kuhamasisha wazazi wao zaidi kuipanda majumbani kwao," anasema Juliana.

Anaongeza kuwa MJUMITA inalenga kufundisha watoto na imetoa wito kwa walimu wa shule ya msingi Ulaya Mbuyuni na Sekondari ya Ukwiva kuwa kila shule ichague wanafunzi wanne ili wapewe mche mmoja wamwagilie kwa zamu na kuistawisha.

Vilevile anasema, kila mwanzoni wa mwezi walimu wafanye ukaguzi wa miche kwa kila kundi la watoto wanne na kila mche watoe namba na majina ya wale watoto wanaohudumia na watakao fanya vizuri, MJUMITA itazipa tuzo shule bora.

Kabla ya mradi walitoa mafunzo kwa kamati ya maliasili yenye wanachama 12 na wananchi waliopo maeneo ya jirani, viongozi wa serikali ya kijiji, maofisa tarafa, watendaji kata, madiwani, wanafunzi na wajumbe wa halmashauri ya kijiji, walimu na waratibu wa elimu kuanzisha vitalu vya miche, kuzalisha na kuipanda.

Lengo kuu ni kuvutia wananchi kuendelea kupanda miti katika maeneo yao ikiwemo ofisi ya mtendaji wa kata, tarafa, maeneo ya jamii, ofisi za kata na vijiji, mahakama, makanisani pamoja na vijiji jirani na ofisi zao.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ulaya – Mbuyuni, Ramadhan Said (mwenye tai) akiwa na wanafunzi wakishuhudia uzinduzi wa kampeni. Anayepanda mti ni Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Majid Mwanga. **PICHA: MWANDISHI WETU**

> "Kabla ya kupata mafunzo, tulianza kufanya tathmini ya mabadiliko ya tabianchi na jinsi wanajamii wanavyohimili.

MAZINGIRA

# Tambua misitu ilivyo moyo wa nishati mijini na vijijini



Kuni na mkaa nishati inayotumika kila mahali kupikia chanzo chake ni misitu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Dk. Felician B Kilahama**

NAWAPONGEZA wasomaji na wengine wenye kiu ya kuongeza maarifa na ufahamu zaidi kuhusu rasilimali misitu na nyuki na umuhimu wake katika maisha na mazingira yanayowazunguka. Katika makala ya Jumanne iliyopita (TESA) nilifafanua umuhimu wa misitu kwa kuhifadhi ardhi na udongo na uhusiano wake na maji ya mvua.

Makala hii imejikita zaidi kwenye sekta ya nishati kwa kuzingatia mchango wa misitu katika upatikanaji wa nishati hasa kuni na umeme kuendeleza maisha ya Watanzania vijijini na mijini.

Misitu ikitazamwa kama miti jinsi ilivyo na vilivyomo ndani yake, wengi wetu na kwa mtazamo wao, wataona ni kitu cha kawaida na kukosa hisia za kuwafanya washtuke inavyoharibiwa au kutoweka kwa kasi ya kutishia uhai wa Watanzania.

Kuna uhusiano mkubwa kati ya misitu na upatikanaji wa nishati kwa matumizi jumuishi nyumbani, viwandani na biashara au uchumi kwa ujumla. Kwa takribani miaka 60 ya uhuru upishi nyumbani unategemea sana kuni na mkaa kama chanzo muhimu kupikia chakula.

Kwa kiasi kikubwa kuni zikitumika vijijini na mkaa mijini.

Kwa takribani miaka 50 iliyopita asilimia 90 ya nishati nchini ilikuwa inatokana na tungamotaka (biomass) ambayo ni misitu wakati asilimia ndogo inapatikana kutoka vyanzo vingine kama umeme, mafuta ya taa, gesi ya mitungi (LPG) na nishati jadidifu kama jua (sola), biogesi, na biriketi (briquettes) vyanzo hivi vikichangia kwa kiasi kidogo sana.

> Kadhalika, itaweza kuona ni kwa kiasi gani matumizi ya kuni vijijini yamepungua na iwapo vyanzo vingine vitakuwa vinatumika kupika chakula.

Misitu ya asili imekuwa ndiyo kimbilio la wengi kupata kuni kuzalisha mkaa; wakati vijijini kuni siyo zao la biashara kama ilivyo kwa mkaa mijini ingawa pia kuni zinauzwa na kutumika kwa shughuli mbalimbali za biashara hasa kwa wajasiriamali mathalani kupika na kukaanga vyakula, kuchoma nyama, samaki na vitafunwa.

Mkaa ni moja ya zao la misitu lenye biashara kubwa nchini. Mwaka 2010 Benki ya Dunia(WB) ilitoa taarifa iliyoonyesha kuwa biashara hiyo ilifikia Dola za Marekani takribani milioni 650 .

Mkaa mwingi ulikuwa ukitumika sana Dar-Es-Salaam na mwingine kupelekwa Zanzibar na kwamba kwa sasa kuna ongezeko la matumizi ya mkaa katika majiji ya Arusha, Mbeya, Mwanza na Tanga pia miji yote nchini wanategemea zaidi mkaa kupikia chakula na matumizi mengine ukilinganishwa na umeme, gesi na nishati jadidifu.

Ingawa kumekuwapo na matumizi ya gesi ya LPG na gesiasilia pamoja na umeme au nishati jadidifu kiwango chake cha matumizi hakiwezi kulinganishwa na mkaa. Vijijini pia matumizi ya kuni kupikia, kukausha tumbaku, kuchoma matofali na viwandani, hivyo, bado kuni na mkaa vinawakilisha sehemu kubwa ya matumizi ya nishati nchini.

Pengine matokeo ya sensa itakayoanza Agosti 23, 2022 itakapokamilika na takwimu kuweka bayana Watanzania watafahamu kwa uhakika, nafasi ya kuni na mkaa itakuwa imeshuka kwa kiasi gani kwa kulinganisha na asilimia 90 ya miaka iliyopita.

Kadhalika, itaweza kuona ni kwa kiasi gani matumizi ya kuni vijijini yamepungua na iwapo vyanzo vingine vitakuwa vinatumika kupika chakula.

Hili nathubutu kulitaja kwa sababu kwa kipindi cha takribani miaka 10 iliyopita serikali, kwa makusudi ilifanya kazi kubwa ya kusambaza umeme vijijini kwa gharama nafuu. Takwimu zinaonyesha kuwa mpaka sasa imetumia Shilingi trilioni tatu kusambaza umeme vijijini nchini kote.

Kwa awamu ya tatu inayoendelea kutekelezwa Shilingi trilioni 1.2 zitatumika.

Changamoto iliyopo ni gharama kubwa za vifaa vya kumwezesha mtumiaji wa umeme au gesi kupika chakula la sivyo umeme utatumika kuwasha taa nyakati za usiku. Sehemu kadhaa katika vijiji vilivyopata umeme, wapo wachache wanaonufaika zaidi kwa shughuli za kibiashara mfano, kutengeneza na kuuza madirisha ya vyuma, kutengeneza vitanda vya chuma na mahitaji mengine kulingana na wateja.

Tukiweka kando suala la nishati ya kupikia, misitu pia inachangia katika upatikanaji wa umeme unaotokana na nguvu ya maji (hydropower) mfano, kupitia mabwawa ya Mtera, Kidatu, Kihansi na Nyumba ya Mungu. Sehemu nyingine ni Rusumo mpakani mwa Tanzania na Rwanda lakini pia bwawa kubwa la Mwalimu Nyerere likikamilika litaiwezesha Tanzania kuzalisha megawati 2,100 za umeme.

Kwa hali hiyo rasilimali misitu hasa misitu lindimaji, ambayo ni vyanzo vikuu vya maji yanayotirikika kwenye mito kama Ruaha Mkuu ambao ni chanzo kikuu cha maji katika mabwawa ya Mtera na Kidatu kwa udi na uvumba lazima misitu hiyo isimamiwe na kutunza ipasavyo.

Mto Ruaha Mkuu ukiungana na Mito ya Kihansi na Kilombero, unakuwa Mto Rufiji ambako Bwawa la Mwalimu Nyerere linajengwa (eneo la Stigler's Gorge). Hatua madhubuti itabidi zichukuliwe kuhakikisha shughuli za kibinadamu hazifanyiki ndani ya ukanda wa mita 60 au 30 (kutegemeana na ukubwa na umuhimu wa mto husika) kutoka kwenye kingo za mto.

Ukanda wa aina hiyo ni muhimu ili kuzuia mito kujaa udongo na kusababisha vina vya mito kupungua, hatimaye kupelekea kutokea mafuriko katika maeneo mbalimbali na maji kuwa majitaka kiasi cha taifa kutumia fedha nyingi kuyasafisha kabla hayajasambazwa kwa watumiaji vijijini na mijini.

Nashauri kuwa suala hili muhimu siasa na maslahi binafsi viwekwe kando na wataalamu wa uhifadhi na mazingira pamoja na viongozi wote wa ngazi mbalimbali, ikiwamo wabunge, watunga sera na wafanya maamuzi lengo liwe ni moja, kuona mito inatiririsha majisafi mwaka mzima kwa maslahi ya taifa na watu wake.

Vilevile, umeme upatikane kwa gharama nafuu kuwezesha familia nyingi kuutumia kupikia chakula na matumizi mengine ya nyumbani. Misitu ya asili isiposimamiwa na kutunzwa ipasavyo, tusishange kuona au kusikia Bwawa la Mwalimu Nyerere halipati maji toshelezi ya kuzalisha umeme wa uhakika.

Tuzibe mianya yote inayolenga kuwanufaisha watu wachache kupitia sekta binafsi kutokana na kuzalisha umeme kwa kutumia jenereta zinazotumia mafuta au gesi kwa gharama kubwa. Hili linawezekana iwapo serikali itatoa kipaumbele katika kuhifadhi, kutunza na kusimamia misitu ya asili bila ya kigugumizi wala kufikiria maslahi binafsi. Badala yake mkazo uwe maslahi Tanzania kwa maendeleo ya taifa.



# Mwenge wabaini madudu miradi

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

MWENGE wa Uhuru umebaini kuwapo na dosari mbalimbali kwenye miradi 64 yenye thamani ya Sh. bilioni 12.5 iliyotembelewa.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, alibainisha hayo juzi kwenye makabidhiano ya Mwenge uliokuwa ukitokea mkoa wa Singida na kuingia Dodoma katika kijiji cha Nagulo, Wilaya ya Bahi.

Katambi alisema hadi sasa Mwenge umepita katika Halmashauri 135 kati ya 195 nchini na kutembelea miradi 941 yenye thamani ya Sh. bilioni 551.7.

"Miradi 64 kati ya hiyo ilikuwa na changamoto ya ufundi na utaalamu na thamani yake ni Sh. bilioni 12.5. tumeagiza kufanyia marekebisho ili kukidhi vigezo," alisema Katambi.

Alifafanua zaidi ya kuwa Mwenge wa Uhuru ni jicho la Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora hivyo mradi unapaswa kutekelezwa ipasavyo ili wananchi wafaidike nayo.

Naibu waziri pia alisema Sh. milioni 847.6 zimekusanywa kwenye halmashauri kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya vijana ambapo fedha hizo zilitolewa na serikali kuu na hazikuwa zimerejeshwa.

Alisema halmashauri za Dodoma bado zinadaiwa Sh. bilioni 150 na kuzitaka kuhakikisha zinarejesha kabla Mwenge haujaondoka mkoani humo.

Naye Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Sahili Geraruma, alisema halmashauri za Dodoma zinatakiwa kukusanya Sh. milioni 150.

"Halmashauri zinaelekezwa kurejesha fedha kabla Mwenge wa Uhuru haujafika katika halmashauri hizo, kwa mustakabali wa maendeleo ya vijana, hautaondoka kwenye halmashauri mpaka fedha zilipwe," alisema.

**"Miradi 64 kati ya hiyo ilikuwa na changamoto ya ufundi na utaalamu na thamani yake ni Sh. bilioni 12.5. tumeagiza kufanyia marekebisho ili kukidhi vigezo," alisema Katambi.**

# Timu yaundwa kutafiti umahiri, ujuzi mafunzo ya elimu ya ufundi

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

SERIKALI imeunda timu ya wataalamu ya kufanya utafiti fuatilizi wa masuala ya umahiri, ujuzi na waajiri kwenye elimu inayotolewa na vyuo vya ufundi stadi (VETA) ili kusaidia maboresho ya mitaala yake.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alitangaza timu hiyo jijini hapo kwa wadau wa elimu wa mapitio ya maoni juu ya uboreshaji wa sera ya elimu na mabadiliko ya mitaala ya elimu msingi.

Alisema lengo la utafiti huo ni kuhakikisha elimu ya ufundi inaendana na mahitaji ya soko la ajira linalohitajika nchini.

Aliwataja wataalamu hao kuwa ni kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) ambao ni Dk. Hamisi Mwinyimvua, Prof. Deograsias Mushi, Dk. John Chegere, Dk. Claude Maeda na Dk. Ibrahim Kadigi.

"Tunatoa elimu ujuzi lakini hatujaangalia inakidhi vipi mahitaji ndiyo maana tumeunda hii timu. Kama kuna mtu ana maoni awe mhitimu au mwajiri, atoe maoni kwenye hii timu na uwezeshaji wa timu unafanywa na NACTVET na kusimamiwa na wizara," alisema.

Alisema idadi ya wahitimu kutoka vyuo hivyo nchini imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2016 wahitimu walikuwa zaidi ya 170,000 na sasa kufikia zaidi ya wahitimu 320,000.

"Wataenda kuchukua taarifa za wahitimu watafuatilia kujua wapo wapi na wanafanya nini, lakini kuna kozi ambazo zinahitajika kwenye hoteli lakini kwa vyuo vya VETA hazitolewi tu-angalie," alisema.

Alisema ni muhimu kwenye mapitio ya mitaala ya elimu ya ufundi kuangalia ujuzi unaotolewa kama una tija.

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Dk. Francis Michael, alisema wizara inaendelea na utaratibu wa ushirikishwaji katika kuboresha sekta ya elimu nchini.

Naye Mwenyekiti wa Timu hiyo, Dk. Mwinyimvua, alisema utafiti huo unafuatilia wahitimu wa miaka mitano wa VETA kutoka mwaka 2017 hadi 2021 ambapo unaangalia masuala mbalimbali ikiwamo kujua vikwazo wanavyopambana navyo wahitimu wanapoenda kwenye soko la ajira ili kuboresha.

"Tunataka kujua kama elimu au ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira au mahali pa kazi unaendana na elimu au mafunzo yanayotolewa na vyuo husika," alisema.

Dk. Mwinyimvua alisema watahoji wahitimu wasiopungua 4,500 katika mikoa yote ya Tanzania Bara na ripoti ya mwisho itawasilishwa wizarani ifikapo Novemba, mwaka huu, tayari kutumika kwenye uamuzi mbalimbali wa kisera.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kushoto), akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, wilayani Bahi jana, kwa ajili ya kuanza kuukimbiza mkoani humo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Asasi zapewa bil. 4/- utatuzi wa migogoro na utawala bora

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

ASASI za Kiraia (AZAKI) 89 kati ya 1,200 zilizowasilisha maombi ya ruzuku kwa Shirika la Foundation for Civil Society (FCS), zimepatiwa Sh. bilioni nne kwa ajili ya miradi mbalimbali ya utawala bora na utatuzi wa migogoro.

Akizungumza jana katika warsha ya usimamizi wa ruzuku kwa AZAKI hizo zilizopata ruzuku, Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Francis Kiwanga, alisema miradi itakayotekelezwa chini ya programu za utawala bora ni kwenye sekta za maji, elimu, afya na kilimo, usawa wa kijinsia, ujumuishwaji wa vijana na watu wenye ulemavu kwa mwaka 2022/23.

"Tumepata wadau 89 wanaotoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar na kazi kubwa itakayofanyika ni kusukuma ajenda ya utawala bora hapa nchini," alisema.

"Eneo lingine la utawala bora ni vita dhidi ya ukatili wa kijinsia lakini kundi la vijana, kuhakikisha rasilimali zinazotolewa na serikali na wadau wengine, kweli ziwafikie makundi hayo na watu wenye mahitaji maalum," aliongeza.

Alitaja eneo lingine litakalofanyiwa kazi na asasi hizo ni kutunza amani na kutatua migogoro Tanzania Bara na Visiwani.

"Tunafahamu sasa hivi kumekuwa na ongezeko la migogoro katika rasilimali kama tunavyoona sehemu nyingine wakulima na wafugaji, wamekuwa na migogoro ambapo kuna zaidi ya taasisi 10 zitafanya kazi ya utatuzi wa migogoro nchini," alisema.

Alisema shirika hilo kazi yake ni kutafuta raslimali na kuziweka pamoja ili kusukuma ajenda ya maendeleo na kuondoa umaskini.

"FCS imepitisha mpango mkakati mpya wa mwaka 2022-2026 ambao unataka kuona wananchi waliowezeshwa, wastahimilivu, wanaowajibika na wanaopata haki za kiuchumi, kijamii na kuboresha ubora wa maisha yao. Tutafanikisha malengo yetu kwa kuchangia maendeleo endelevu na shirikishi nchini Tanzania kwa kuimarisha uwezo, kugawana rasilimali, na ushirikiano wa kimkakati na AZAKI, vikundi vya jamii pamoja na watendaji wengine wa maendeleo," alisema.

Naye Meneja Programu Utawala Bora wa FCS, Edna Chilimo, alisema asilimia 70 ya asasi zilizopata ruzuku ni wadau wapya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali la TAWSEI kutoka mkoa wa Tanga, Bernadethe Choma, alisema fedha hizo zitasaidia kujenga uelewa wa jamii na kuboresha afya.





# Tume ya Maendeleo Ushirika kuwa benki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika inakusudia kupanua wigo wake na kuwa benki ya kitaifa ili kuvisaidia vyama vya ushirika na wanachama wake kupata huduma bora karibu na maeneo yao.

Mtendaji Mkuu wa tume hiyo na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, alibainisha hayo juzi jijini Mbeya alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mikakati yao.

Alisema lengo la benki hiyo ni kuvisaidia vyama vya ushirika kupata mitaji na kuondokana na utaratibu wa kukopa mitaji kutoka kwenye benki za kibiashara, akisisitiza kuwa utaratibu huo unafifisha nguvu za vyama vyao.

Vilevile, alisema vyama hivyo vinapokopa fedha kutoka kwenye benki zingine, vinakuwa vinanufaisha benki hizo badala ya kujinufaisha wao wenyewe kupitia benki yao ambayo alisema inawasaidia moja kwa moja bila masharti magumu.

Dk. Ndiege alisema vyama vya ushirika nchini viko vingi na hivyo vikiungana na kuunda benki, vitakuwa na benki iliyo imara zaidi kulinganishwa na benki zingine ambazo kwa sasa zinategemea shughuli zao.

"Kwa sasa tunahitaji tuwe na mtaji ambao unafikia Sh. bilioni 15 kwa ajili ya kuimarisha benki yetu na tumeshafanya mazungumzo na serikali kwa ajili ya kuifufua benki hii, kilichobaki ni sisi kupata huo mtaji ili tuanze kutanua wigo," alifafanua.

Alisema serikali imekuwa ikiweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha ushirika nchini ikiwa ni pamoja na kuajiri maofisa ushirika kila wilaya pamoja na warajisi wa vyama vya ushirika katika ngazi za mikoa nchini kote. Alikumbusha kuwa hivi karibuni serikali ilikabidhi zaidi ya pikipiki 130 kwa maofisa ushirika nchini kote ili ziwasaidie kuvifikia vyama mbalimbali vya ushirika kwenye maeneo yao ya kazi.

Alisema utaratibu wa serikali kutaka mazao mbalimbali yauzwe kwa njia ya ushirika unalenga kuwasaidia wakulima wenyewe, lakini uelewa wa baadhi ya wakulima ni mdogo na hivyo wataendelea kutoa elimu.

Aliwataka viongozi mbalimbali wa serikali kuhakikisha wanasaidiana na tume hiyo kuhamasisha wakulima kuuza mazao yao kupitia vyama vya ushirika.

"Baadhi ya mazao ambayo mpaka sasa yanauzwa kupitia vyama vya ushirika ni kahawa, kakao, korosho, tumbaku na mazao mengine ya biashara. Tunaomba wakulima waendelee kuunda vyama vyao," alisema.

Dk. Ndiege alisema wanaendelea na mikakati ya kuimarisha vyama vya ushirika kwa kutoa elimu ya ushirika kwa wananchi na vyama vyao ili waviendeshe kwa kufuata misingi ya kisheria.

Alisema viongozi wa vyama vya ushirika wamekuwa wakipatiwa mafunzo ya uongozi wa ushirika ili waviongoze vyama vyao kwa kufuata misingi ya utawala bora pamoja na mafunzo ya matumizi bora ya rasilimali.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako (wa pili kulia), akiangalia majani ya chai, alipotembelea Kiwanda cha Chai Mponde mkoani Tanga juzi. Kiwanda hicho, kinachomilikiwa kwa ubia kati ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), ukarabati wake umekamilika kwa asilimia 95% na uzalishaji unatarajiwa kuanza mwishoni mwa Septemba mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbolea ya ruzuku yaanza kutolewa kwa wakulima

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imeanza kutekeleza mpango wa serikali wa kutoa mbolea ya ruzuku kwa wakulima ili kuinua kiwango cha uzalishaji na kuwainua wakulima kiuchumi.

Kaimu Meneja wa TFRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Michael Sanga, alibainisha kuanza kwa utekelezaji wa suala hilo alipozindua mpango huo katika Kijiji cha Sogeza Kata ya Isongole wilayani Rungwe juzi.

Alisema wafanyabiashara wameandaliwa kwa ajili ya kusambaza mbolea hiyo kwa wakulima na watahakikisha msimu unaanza wakati mbolea imefika maeneo yote nchini ili wakulima wawe tayari kwa msimu mpya wa kilimo.

Alisema wamefanya ukaguzi na kubaini wafanyabiashara wameshaanza kuingiza mbolea mapema na wameshapatiwa bei elekezi za mbolea nchi nzima.

"Wafanyabiashara wetu wamejipanga vizuri, kwenye maghala kuna mbolea ya kutosha kwa ajili ya kuziuza kwa wakulima na kufanikisha lengo la serikali la kuwapa nafuu wakulima," alisema.

Sanga alisema wakulima walikuwa wanapata shida kununua mbolea kwa bei ya juu misimu iliyopita kwa kuwa hakukuwa na ruzuku ya serikali na hivyo akawahakikishia wakulima kwamba mwaka huu wataipata kwa bei nafuu.

"Jambo la msingi kwa sasa wakulima wanatakiwa kujisajili katika madaftari ili wawe sehemu ya wanufaika maana kwa utaratibu huu mpya, hakuna mkulima atauziwa mbolea bila kujisajili, serikali imeanzisha utaratibu huu ili kuwapunguzia mzigo wakulima," alisema Sanga.

Baadhi ya wakulima wilayani Rungwe waliishukuru serikali kwa kuanzisha mpango huo wa ruzuku, wakiamini utawasaidia kupunguza gharama za uzalishaji tofauti na ilivyokuwa msimu uliopita.

Mchungaji Msafiri Sumbo, mkulima wa viazi na mahindi katika Kijiji cha Iwili, alisema wakulima wengi walianza kukata tamaa kuzalisha baadhi ya mazao kutokana na bei ya mbolea kuwa juu.

Alisema kuwa msimu uliopita hata tija ya uzalishaji ilipungua kutokana na wakulima kutomudu bei ya mbolea na hata gharama za maisha zilianza kupanda kwa kasi kutokana na vyakula kuuzwa kwa bei ya juu.

"Mbolea ilikuwa inauzwa kwa bei ya juu mno, mbolea za kupandia huku kwetu tulikuwa tunanunua kwa zaidi ya Sh. 120,000, jambo ambalo lilikuwa linatufanya tushindwe kumudu, kuna watu huwa tunategemea kuuza mazao ili wawasomeshe watoto sasa kazi ilikuwa ngumu," alisema Mchungaji Sumbo.

Haruna Obeza, mkulima wa viazi, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa mpango huo wa mbolea ya ruzuku kwa maelezo kuwa utaratibu huo umeonyesha namna ambavyo serikali inawajali watu wake.

Agosti 8 mwaka huu, Rais Samia alizindua mpango wa ruzuku ya mbolea kitaifa katika Viwanja vya John Mwakangale alipofunga maonyesho ya wakulima, maarufu Nanenane, na kuagiza mbolea iliwafikie wakulima Agosti 15 mwaka juu, yaani (juzi).

Akitoa maelezo ya mbolea hiyo, Waziri wa Kilimo, Husein Bashe, alisema mbolea itakayouzwa kwa bei ya juu zaidi ni ya bei ya Sh. 70,000 na ya bei ya chini itakuwa Sh. 60,000.

## Machinga walia kutokuboreshwa walikohamishiwa

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BAADHI ya wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, waliohamishiwa katika eneo la uwanja wa ndege wa zamani jijini Mbeya, wameiomba serikali kuboresha mazingira kabla ya kuanza kwa msimu wa mvua kwa kuwa eneo hilo hufurika maji.

Wafanyabiashara hao wameomba mifereji ya maji kuchongwa mapema ili kuepusha maji kutuama kwenye eneo hilo na kusababisha wateja kuwakimbia.

Wakizungumza na Nipashe jana, wafanyabiashara hao walisema walihamishiwa kwenye eneo hilo wakitokea kwenye maeneo mbalimbali ambayo yalikuwa mazuri kwao kibiashara.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Joshua Kamwela, alisema awali alikuwa anafanya biashara zake katika eneo la Kabwe lakini serikali iliwaondoa huko ikiwahakikishia kwamba mazingira hayo ya uwanja wa zamani yataboreshwa.

Alisema kwa sasa pamoja na kwamba wameshahamishiwa huko, hakuna kinachofanyika kwenye eneo hilo zaidi ya kuendelea kupewa matumaini kuwa litaboreshwa.

"Kama unavyoona hili eneo mwelekeo wa maji hauonekani, maji yote yanakusanyika hapa, tunaomba kama kweli mpango huo upo, basi wafanye haraka ili mvua itakapoanza kunyesha, mazingira yakutwe yakiwa na miundombinu ya kupitisha maji," alishauri.

Neema Mwakabungu alisema katika eneo hilo, baadhi ya wajasiriamali wanapanga bidhaa zao chini kutokana na kutokuwapo kwa vichanja wa hivyo mvua ikianza kunyesha, watashindwa kufanya biashara.

Alisema kwa sasa wameshaanza kujengewa majengo kwa ajili ya biashara zao lakini kama hayatakamilika mpaka kipindi cha mvua kinaanza, watashindwa kufanya shughuli zao.

Hivi karibuni, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima, aliuagiza uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuwaboreshea mazingira wajasiriamali hao ili wafanye biashara kwenye mazingira rafiki.

Dk. Gwajima alisisitiza viongozi hao kuanza na eneo la wauza maziwa ambao walihamishwa kutoka eneo la Mwanjelwa na sasa wanafanya biashara kwenye eneo ambalo siyo safi.





# Wizara, taasisi zaingia ubia utatuzi kero maji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar imeingia makubaliano na Taasisi ya Global Water Partnership ya Tanzania Bara kushirikiana kutatua kero zinazowakabili wananchi katika kupata huduma ya maji.

Hafla ya utiaji saini makubaliano hayo ilifanyika jana katika ofisi za wizara hiyo mjini Zanzibar, Waziri wake, Shaibu Hassan Kaduara, akikiri Zanzibar inakabiliwa na shida katika utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi.

Alisema kupitia ushirikiano huo, watapata msaada kufanya utafiti kubaini maeneo yenye maji ya uhakika ili kupunguza uchimbwaji wa visima kiholela na kupunguza malalamiko ya wananchi wanaochukuliwa maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa visima.

Kaduara alisema kutokana na tatizo la maji Zanzibar kuwa la muda mrefu na kero kwa wananchi, serikali kupitia wizara hiyo iko tayari kushirikiana na Global Water Partnership ili kuondosha tatizo hilo ambalo limeathiri maeneo mengi.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Global Water Partnership Tanzania, Ngwisa Mpembe, alisema ni vyema Zanzibar waitumie fursa hiyo ya makubaliano na kuwanufaisha kwa kupatiwa wataalamu watakaowajengea uwezo wafanyakazi wa Wizara ya Maji Zanzibar pamoja na kufanya utafiti wa vyanzo vipya vya maji.

Alisema wataboresha miundombinu katika sekta ya maji kwa ujenzi mzuri wa visima ili kuondosha tatizo la maji Zanzibar linalokwamisha harakati za maendeleo.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Dk. Victor Kongo, alisema wameamua kuisaidia Zanzibar ili kuijenga katika sekta ya maji, hivyo kujisimamia wenyewe katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Katibu Mkuu Joseph Kilangi, alisema ushirikiano huo utaimarisha udugu wao na kuwa chachu na kuchochea upatikanaji wa huduma ya maji.

## Wajasiriamali wapewa mbinu kuinuka kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Abeida Rashid Abdallah, amewataka wajasiriamali kujifunza mambo mapya kutoka kwa wenzao ili kubadilishana ujuzi na uzoefu katika nyanja tofauti.

Alibainisha hayo jana alipozungumza na kikundi cha wajasiriamali cha Tufahamiane Women Group kinachojishughulisha na usafi wa mazingira na utengenezaji wa mkaa kilichoko Kizimkazi, Mkunguni, Wilaya ya Kusini Unguja.

Naibu Katibu Mkuu huyo alisema kufanya hivyo kutawasaidia wajasiriamali hao kujua vitu mbalimbali na kuwa na ujuzi zaidi wa kujikwamua kimaisha.

"Tuwe na tabia ya kujifunza mambo mengine kutoka kwa wajasiriamali waliofanikiwa, hili litatufungua zaidi kwenye shughuli zetu lakini pia kuzitumia fursa zilizoko," alisema.

Abeda alikemea vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia vinavyofanywa na baadhi ya wanaume katika familia, akiwataka wazazi kuwa makini katika malezi ya watoto wao.

Pia alitumia fursa hiyo kuwataka wazee wenye umri wa kuanzia miaka 70 ambao hawajaandikishwa katika pensheni ya jamii inayotolewa kila mwezi, wajiandikishe ili kuingizwa katika utaratibu huo wa kupatiwa pensheni.

Katibu wa Kikundi cha Tufahamiane Women Group, Talha Mussa Haji, alisema awali kikundi chao kilikuwa cha elimu ya watu wazima na sasa wanafanya kazi nyingi, ikiwamo utengenezaji wa vyungu.

"Kwa sasa kikundi chetu kinajishughulisha na ukusanyaji wa taka za majani ya mua, nazi na kutengeneza mkaa wa kupikia ambapo moshi wake hauna madhara," alisema.

Mwakilishi wa taasisi inayozalisha mkaa ya United for Green (UGF), Nasriya Khamis Salum, alisema mpaka sasa vikundi vitatu vya wajasiriamali tayari vimepatiwa mafunzo ya utengenezaji wa mkaa huo unaohifadhi mazingira.

Alisema lengo la taasisi hiyo ni kuvisaidia vikundi vya wanawake katika utunzaji wa mazingira kwa kutengeneza mkaa kutoka kwenye taka za majani.




Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui (kulia), akimkabidhi zawadi maalum Mbunge wa Chama cha Social Democratic cha Ujerumani, Tina Rudolph, alipomtembelea ofisini kwake, Mnazi Mmoja, Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mazrui aahidi neema bima ya afya Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, amesema Serikali ya Ujerumani imekusudia kuanzisha mfuko wa bima ya afya ambao utasaidia wananchi kuwapunguzia gharama za matibabu na kupata huduma bora nchini.

Alitangaza neema hiyo jana ofisini kwake Mnazimmoja alipotembelewa na wabunge wa Chama cha Social Democratic cha Ujerumani kujadili namna ya kupunguza na kumaliza maradhi mbalimbali ikiwamo kifua kikuu, VVU/Ukimwi, homa ya ini na malaria.

Alisema ni muhimu kutumia bima na kutasaidia kuinua hali za wanyonge ambao hawawezi kumudu gharama kubwa za matibabu, hivyo kupunguza ugumu wa gharama za matibabu kwa wananchi wa Zanzibar.

Aidha, Mazrui alisema ushirikiano uliopo kati ya Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Ujerumani unazidi kuimarisha sekta ya afya na umesaidia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza maradhi mbalimbali.

"Ujio wa wabunge hawa utaimarisha ushirikano kati yetu na Wajerumani na utasaidia zaidi kuimarisha sekta ya afya katika kukabiliana na maradhi mbalimbali.

"Mfuko huu tukiuzindua, utatuinua kimatibabu na wananchi wengi hatumudu gharama kubwa za matibabu," alisema waziri huyo.

Mazrui aliwahakikishia wabunge hao kuwa msaada wao wanaoutoa, unatumika vizuri katika kuimarisha matibabu kwa kununua vifaa tiba ambavyo vinasaidia wagonjwa na wananchi kwa ujumla.

Wabunge hao waliahidi kuendeleza ushirikiano wao kwa lengo la kustawisha afya za wananchi wote wa Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOSEPH SIMON SIMKOKO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota **RAV 4** namba za usajili **T 785 DGD.** Chassis no. **ACA210094607**, Engine **No.1AZ0296676.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/326671/2022**.

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**DOTTO DAVID PETER** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **OMARY HARUNA MBWANA** aina ya Bajaj Boxer namba za usajili **MC 184 CJV.** Chassis no. **MD2A21BY9KWF99193.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/168851/2022.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**SAMSON PAULO BALAMA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya **PIKPIKI** mali ya **MOHAMMED ENTERPRISES(T) LTD** yenye namba za usajili **MC 104 CDZ** Chasis Namba: **MD2A21BY6JWJ95747** Engine Namba: **PFZWJJ57352** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/325094/2022.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA MAOMBI NAMBA 35/2021**

**AHAMAD SELEMAN MATEKA**

**(Msimamizi wa mirathi ya Seleman MATEKA)-----MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**1.MWANAISHA FARAJI**
**2.ZIADA FARAJI**
**3.NASSORO FARAJI**
**4.CHAMA CHA WAFANYABIASHARA NA MNADA SONGEA**
**5.FARAJA MAKUKULA------WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Wajibu maombi namba nne na tano mnataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yenu.Hivyo basi mnatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wenu,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 2/09/2022 saa 2.00 asubuhi.Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zenu za utetezi.

Kumbuka pia kushindwa kwenu kufika shaurini kutapelekea baraza hili usikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wenu.
Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo 12/08/2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SONGEA

## KUPOTEA KWA VYETI



**GLORY GIFT TEMU,** anatangaza kupotelewa kwa vyeti vya elimu ya sekondari, kidato cha nne na sita vyenye index namba, **S0869-0012 October 2005** Mboni Secondary school, **P1475-0587 October 2006** Perfect Vision Secondary school centre, **S0731-0550 February 2009** Makongo Secondary school Kwa yeyote atakaye viona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **RB/MBE/KYE/ 325527/2022**


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676**

**Kwa Habari Moto-moto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Milipuko yashuhudiwa Crimea, Ukraine yatahadharisha raia wake

**Kyiv,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amewashukuru wote wanaopinga uvamizi wakiwamo wananchi wake ambao wamevisaidia vikosi vya jeshi la nchi hiyo, idara ya ujasusi na vikosi maalum katika harakati za kuwadhibiti wavamizi.

Akizungumza usiku wa kuamkia jana, saa chache baada ya kambi ya kijeshi katika eneo linalokaliwa kimabavu na Russia Crimea kushambuliwa kwa milipuko kadhaa. Zelensky alisema chanzo cha milipuko hiyo inaweza kuwa na sababu mbalimbali ikiwamo uzembe.

"Kila siku tunasikia taarifa kuhusu milipuko katika eneo linalokaliwa na wavamizi. Ninawaomba watu wa Crimea na majimbo mengine ya kusini mwa nchi ambayo pia yanakaliwa, Donbas na Kharkiv kuwa makini sana," alifafanua Zelensky.

Zelensky aliwatolea wito wananchi wa Ukraine kutozisogelea kambi za kijeshi zinazodhibitiwa na jeshi la Russia na maeneo yote ambayo jeshi hilo linahifadhi silaha, vilipuzi na vifaa vingine vya kijeshi.

Nayo Wizara ya Ulinzi ya Russia ilisema kuwa hujuma ndiyo chanzo cha milipuko hiyo katika ghala la jeshi kwenye jimbo la Dzhankoy huko Crimea.

Ukraine haijathibitisha rasmi kama inahusika na milipuko hiyo, lakini iwapo vikosi vya Ukraine vinahusika, inaonesha kuwa inaweza kufanya operesheni za siri dhidi ya adui yake.

Guterres kwenda Ukraine na Uturuki wakati huo huo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, anatarajiwa kuizulu Ukraine leo kwa ajili ya kukutana na Zelensky pamoja na Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan.

Viongozi hao wanatarajiwa kujadiliana kuhusu mkataba wa nafaka unaoiruhusu Ukraine kusafirisha chakula kwenda katika masoko ya dunia ili kusaidia kuupunguza mzozo wa njaa ulimwenguni.

Mkataba huo unasimamiwa na Umoja wa Mataifa na Uturuki.

Msemaji wa Umoja wa Mataifa, Stephane Dujarric, alisema umuhimu wa kupatikana suluhisho la kisiasa katika vita, pia litaibuliwa wakati wa mkutano huo utakaofanyika katika mji wa Lviv ulioko magharibi mwa Ukraine.

Kwa mujibu wa Dujarric, viongozi hao watatu pia watajadiliana hali katika kinu cha nishati ya nyuklia cha Zaporizhzhia kinachodhibitiwa na Russia, ambako nchi hizo mbili zinalaumiana kushambulia kwa makombora.

Guterres pia ataizulu Odesa ambayo ni mojawapo ya bandari tatu zinazotumika kusafirisha nafaka. **DW**

# Ruto aonyesha makali kabla ya kuapishwa

**Nairobi,** KENYA

RAIS mteule wa Kenya, William Ruto amesema mawaziri atakaowateua katika serikali yake watawajibishwa bungeni, kupitia kujibu maswali ya jinsi serikali yao inavyofanya kazi.

Ruto, amewataka wafanyakazi wa umma kutoshiriki katika siasa na badala yake kuwahudumia Wakenya wote bila kupendelea chama, kabila au eneo wanalotoka.

Akizungumza alipokutana na viongozi mbalimbali waliochaguliwa kupitia Muungano wa Kenya Kwanza, Ruto alisema, watabadili sheria za vikao vya bunge kuhakikisha kwamba mawaziri wa serikali yake wanajibu maswali.

Alisema kwamba, haitoshi kwa mawaziri kukutana na kamati za bunge pekee na kwamba ni muhimu wawaeleze Wakenya jinsi serikali yao inavyowahudumia.



Aliongeza, licha ya kuwa serikali yake itakuwa ya kidemokrasia ni lazima iwajibike. Kuhusu wafanyakazi wa umma, Rais huyo mteule alisema anawahakikishia kwamba kazi zao zipo salama na hawatahusishwa tena na masuala ya kisiasa kama ilivyo sasa.

Matamshi ya Ruto yanajiri siku mbili tu baada ya kutangazwa mshindi wa uchaguzi mkuu uliopita ambapo matokeo yake yamezua mvutano katika ya tume ya uchaguzi nchini IEBC.

Siku ya Jumanne makamishna wanne wa tume ya uchaguzi IEBC kati ya saba walipinga matokeo yaliotolewa na mwenyekiti wao Wafula Chebukati, wakidai kwamba yalikabiliwa na kiza kinene.

Makamishna hao walidai kwamba hesabu ya matokeo iliotangazwa na Wafula Chebukati haiingiliani na jumla ya idadi ya kura ya wagombea wanne wa urais.

Vilevile, wanadai kwamba Chebukati hakuwahusisha katika kuhakiki matokeo ya mwisho kabla ya kuyatangaza kwa umma.

Tayari aliyekuwa mpinzani mkuu wa William Ruto na waziri mkuu wa zamani Raila Odinga, ameapa kwenda mahakamani kupinga matokeo hayo akisema kwamba Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi alikiuka katiba kwa kutowahusisha makamishna wake katika mchakato wote wa kutangaza matokeo hayo.

Wakati huo huo, Jaji Mkuu Martha Koome, amepata pigo baada ya Mahakama Kuu kutangaza kuwa ni kinyume cha sheria uamuzi wake wa kuwabana mawakili na walalamikaji kutoa maoni yao juu ya rufani za uchaguzi wa urais wakati bado inasikilizwa na Mahakama ya Juu Zaidi.

Jaji Thande, alipinga kanuni za marekebisho za rufani ya uchaguzi wa urais za Mahakama ya Juu Zaidi za 2022 na kuzitaja kuwa ni kinyume na katiba kwa kutotii matakwa ya ushiriki wa umma.

Sheria hiyo iliyotangazwa miezi miwili iliyopita ilikuwa imekataza maoni ya watu kuhusu rufani ya uchaguzi wa urais mara tu itakapowasilishwa katika Mahakama ya Juu zaidi na wakati bado inasubiri kuamuliwa.

Uamuzi huo umetolewa wakati mgombea wa Muungano na Umoja Kwanza, Raila Odinga, kupanga kwenda mahakamani kupinga hatua ya tume ya uchaguzi kumtangaza Ruto kuwa mshindi wa kura za urais. Pia, ilipiga marufuku uvumi wa matokeo ya rufani hiyo.

CJ Koome, katika kutetea kanuni hiyo, alisema madhumuni ya kanuni hizo ni kulinda uadilifu wa mwenendo wa kesi mahakamani kwa vile kulikuwa na baadhi ya mawakili waliokuwa wakifika mahakamani, kutetea kesi yao na baadaye kupeleka hoja zao kwenye mitandao ya kijamii na kuonesha dharau dhidi ya majaji.

Alidai kuwa, sheria hizo, ambazo zilitangazwa kwenye gazeti la serikali Aprili 12, 2022, zilikusudiwa kuhakikisha hadhi na uhuru wa mahakama unadumishwa na kwamba nia haikuwa kuondoa uhuru wa kujieleza. **BBC**



Helikopta zikisaidia zoezi la kupambana na moto unaoteketeza Hifadhi ya Taifa ya Moncayo karibu na kijiji cha Borja nchini Uhispania jana. **PPICHA: AFP**

# Ujerumani yakemea kauli za Mahmoud Abbas

**BERLIN,** Ujerumani

UJERUMANI imeelezea hasira yake kuhusu matamshi yaliyotolewa na Rais wa Mamlaka ya Palestina Mahmoud Abbas, ambaye aliyesema vitendo vinavyofanywa na Israel dhidi ya Wapalestina ni sawa na mauaji ya kimbari yaliyofanywa dhidi ya Wayahudi.

Balozi mpya wa Ujerumani nchini Israel Steffen Seibert, alisema kauli za Abbas sio sahihi na hazikubaliki.

Ameandika kwenye mtandao wa Twitter kuwa Ujerumani haitawahi kuunga mkono jaribio lolote la kukanusha uhalifu wa mauaji ya kimbari dhidi ya Wayahudi.

Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz, amesisitiza tena kwenye Twitter jana kuwa amekasirishwa na kauli hizo za Abbas alizoziita kuwa zisizovumilika.

Abbas hapo jana aliituhumu Israel kwa kufanya kile alichokiita kuwa mauaji ya kimbari dhidi ya Wapalestina sawa na yaliyofanywa dhidi ya Wayahudi, wakati wa mkutano wa waandishi wa habari na Scholz mjini Berlin.

Abbas alisema Israel imefanya matukio 50 ya mauaji ya kimbari dhidi ya Wapalestina katika maeneo 50 ya Kipalestina tokea mwaka 1947.

# POLISI YATOA SABABU MBILI KUCHEZEA KICHAPO YANGA

**Na Adam Fungamwango**

POLISI Tanzania imetaja sababu mbili za kupoteza mechi ya ufunguzi nyumbani, juzi kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha dhidi ya Yanga.

**Msemaji wa klabu hiyo, Frank Lukwaro, amesema kuwapo kwa idadi kubwa ya majeruhi pamoja na wachezaji wa kigeni kukosa vibali ni sababu ambazo zilikifanya kikosi chao kutokamilika.**

"Ulikuwa mchezo mzuri sana, vijana wamepambana kadri ya uwezo wao, lakini makosa ya mabeki yalisababisha kuruhusu mabao mawili. Unapocheza na timu kama Yanga yenye wachezaji wazoefu, hutumia makosa kama hayo kukuadhibu, lakini kwenye soka hawakutuzidi sana.

Kikubwa ni kwamba tumepoteza mechi sababu kubwa ni kutokuwa na wachezaji wetu muhimu wengi ambao ni majeruhi. Tuna takriban wachezaji saba majeruhi kama Tariq Simba, Fred Tangalu na wengineo ambao walikuwa majeruhi kwa hiyo kikosi chetu bado hakikuwa kimekamilika kwa asilimia mia moja," alisema Lukwaro.

Sababu nyingine aliyoitaja ya kupoteza mchezo huo kwa kufunga mabao 2-1, alisema ni kutokamilika kwa vibali vya wachezaji wa kigeni.

"Baadhi ya wachezaji wa kigeni ambao vibali vyao havijakamilika, tunategemea kuwatumia kwenye mechi nyingine kila kitu kikishakuwa kamili, na nina imani tutafanya vema kwenye mechi yetu inayofuata dhidi ya KMC," alisema.

Juzi, Jumanne Polisi Tanzania ilipoteza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu kwa kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya Yanga, ikiwa ni mara ya kwanza baada ya msimu mmoja kupita. Msimu uliopita iliinyuka KMC mabao 2-0 kwenye mechi ya kwanza ya Ligi Kuu ikichezwa Septemba 29, mwaka jana kwenye Uwanja wa Ushirikika mjini Moshi.

Kipigo dhidi ya Yanga, kimerudia kile kilichotokea msimu wa 2020/21, ilipofungwa bao 1-0, mechi yake ya kwanza dhidi ya Azam FC, Uwanja wa Azam Complex, mechi ikichezwa Septemba 7, 2020.

**AMBAA...**




Mshindi wa kwanza wa mbio za CRDB Marathon kwa wenye uhitaji maalumu zilizodhaminiwa na Vodacom, Shukuru Halfani (katikati), akiwa na washindi wengine pamoja na Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia (kulia), Mjumbe wa Bodi ya CRDB, Martin Warioba (kushoto), na Mkurugenzi wa Kitengo cha Dijitali na Huduma za ziada Vodacom Tanzania Plc, Nguvu Kamando, baada ya kukabidhi zawadi zao, jijini Dar es Salaam. Vodacom iliwazawadia washindi hao kifurushi cha Bima ya "Faraja Yangu" kutoka VodaBima itakayowanufaisha na wategemezi wao ndani ya mwaka mmoja kwa kupata bima ya maisha, fedha za hospitali na bima ya ajali. **MPIGAPICHA WETU**

# *Adam Adam aanika malengo yake Mtibwa Sugar*

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushindwa kuonyesha cheche zake msimu uliopita, mshambuliaji wa Mtibwa Sugar, Adam Adam, amesema malengo yake katika msimu huu wa 2022/23 ni kurejesha ubora wake wa misimu iliyopita kwa kufamani nyavu kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, iliyoanza wiki hii.

Akizungumza na gazeti hili jana, Adam Adam alisema malengo ya msimu huu kwake ni kufanya vizuri na kurejesha ubora wake wa kufunga mabao kama ilivyo kwa misimu ya nyuma kabla ya kutimkia Libya.

Alisema anachotaka ni kuisaidia timu yake kufikia malengo yanayotarajiwa na mashabiki wa Mtibwa Sugar na si ufungaji bora wa ligi hiyo.

"Msimu uliopita sikuwa katika ubora wangu nikiwa na Polisi Tanzania, hii ni baada ya kutoka Libya, msimu huu malengo yangu ni kurejea ubora wangu wa misimu ya nyuma na kuisaidia timu yangu kufanya vizuri zaidi kwenye ligi," alisema Adam Adam.

Alisema katika suala la kurejea katika ubora wake anaamini Mtibwa Sugar ni sehemu sahihi ya yeye kufikia malengo yake ya kurejea katika ubora uliomfanya kupata nafasi ya kwenda kucheza soka la kulipwa nchini Libya katika Klabu ya Al-Wahda ya Tripoli.

Adam Adam amejiunga na Mtibwa Sugar msimu huu akitokea Polisi Tanzania alipocheza msimu uliopita wakati akirejea Tanzania akitokea Libya baada ya kuvunja mkataba na Klabu ya Al-Wahda ya Tripoli.

Nyota huyo alijiunga na Al-Wahda ya jijini Tripoli Juni mwaka jana kwa mkataba wa miaka mitatu kutoka JKT Tanzania, hata hivyo pamoja na mwanzo mzuri, alishindwa kumalizia mkataba wake kurejea nyumbani baada ya msimu mmoja tu wa kucheza Ligi Kuu ya Libya.

Al Wahda ilimsajili Adam baada ya kung'ara katika Ligi Kuu ya Tanzania Bara msimu wa 2019/2020 akifunga mabao 13.



# Bodi ya Ligi Z'bar, klabu watete yao

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BODI ya Ligi Zanzibar imekutana na klabu 16 zinazocheza Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja ili kupanga mambo mbalimbali kueleke msimu mpya wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa bodi hiyo, Hashim Salum, alisema lengo kuu la kukutana nao ni ili kujadili kwa pamoja namna ya kuuanza msimu mpya wa ligi hiyo.

Alisema katika kikao hicho kilichowakutanisha makatibu wa klabu zote za Kanda ya Unguja pamoja na watendaji wa bodi ya ligi, kilikuwa kimelenga kukumbushana umuhimu wa kusoma kanuni za mashindano kwa msimu huu pamoja na klabu kuwasilisha viwanja vyao watakavyovitumia katika michezo ya nyumbani.

Alisema tayari klabu hizo zimewasilisha viwanja zitakavyovitumia katika michezo yao ya nyumbani, hivyo imebaki kwa bodi ya ligi kwa kushirikiana kamati ya leseni ya klabu pamoja na kamati ya mashirikiano kuvipitia na kuvikagua viwanja hivyo.

Aidha, alisema bodi ya ligi itahakikisha inapitisha viwanja ambavyo vinakizi viwango kwa uchezaji ili kuondoa changamoto ya kuuondoa uwanja wakati ligi inaendelea.

"Timu zote 16 zimewasilisha viwanja vyao vya nyumbani, jukumu lililobaki ni kuvipitia viwanja hivyo kabla ya kuviingiza katika ratiba, maana kuna vingine lazima 'vitafeli' na baadhi vitahitaji kufanyiwa maboresho na hasa kwa vile vya mikoani," alisema

Hata hivyo, alisema bodi ya ligi tayari imeshatoa muundo wa ratiba kwa klabu za Ligi Daraja la Kwanza na ratiba kamili ya ligi hiyo itatoka mapema wiki ijayo baada ya kukamilika zoezi la kukaguwa viwanja ambalo litafanywa siku za mapumziko ya wiki hii.

Klabu hizo 16 ni Jang'ombe Boys, Chuoni FC, Kilimani City, Paje Star, Gulioni FC, Mwembe Mkaumbi City, Ngome FC, Mundu FC, New King na Umoja wa Mbuzini.

Nyingine ambazo zimepanda msimu huu ni Raskazone, Black Mamba, New City, Strong File, Ujamaa pamoja na New Boys.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FOFANA NA CHELSEA SAFI

MCHEZAJI Wesley Fofana, 21, wa Leicester City amekubali maslahi binafsi na Chelsea, lakini klabu hizo mbili bado hazijamalizana kuhusu ada - huku klabu hiyo ya Stamford Bridge ikikataa kulipa pauni milioni 85 ili kumnunua beki huyo wa kati wa Ufaransa. ***(Fabrizio Romano)***

### NEWCASTLE KUSAJILI WATATU

KLABU ya Newcastle United imeonyesha nia ya kusajili wachezaji watatu kutoka Chelsea, Callum Hudson-Odoi, 21, Connor Gallagher, 22, na Mmarekani Christian Pulisic (23) - na pia wanamtaka mshambuliaji wa 'The Blues', Armando Broja, 20, raia wa Albania. ***(Telegraph)***

### ODOI KURUHUSIWA

CHELSEA itaruhusu mchezaji anayelengwa na Newcastle United, Callum Hudson-Odoi, 21, kuondoka kwenye klabu, lakini kwa mkopo. Mmiliki mwenza Todd Boehly amemsihi kiungo huyo wa kati wa England kutolazimisha uhamisho wa kudumu. ***(Evening Standard)***

### CASEMIRO ALENGWA MADRID

KIUNGO wa kati wa Real Madrid na Brazil, Casemiro, 30, pia analengwa na Manchester United. ***(Marca)***

### CASADEI KUTUA CHELSEA

CHELSEA imekubali dili la kumsajili kiungo wa kati wa Italia, Cesare Casadei, 19, kutoka Inter Milan kwa pauni milioni 12.6 pamoja na nyongeza ya pauni milioni 4.2. ***(Sky Sports)***

### BARCA HAWANA MPANGO

BARCELONA hawana nia ya kumsajili mlinzi wa pembeni wa Ureno, Diogo Dalot, 23, kutoka Manchester United kama sehemu ya mkataba ambao unaweza kumfanya kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, 25, kwenda upande Old Trafford. ***(Mundo Deportivo)***

### ALLI KUNG'OLEWA EVERTON

KLABU ya Besiktas ya Uturuki inataka kumsajili Dele Alli, 26, wa Everton - iwe kwa mkopo au mkataba wa kudumu. Klabu hiyo ya Ligi Kuu England iko tayari kumruhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa England kuamua anachotaka. ***(Fabrizio Romano)***

### KEHRER KUMALIZANA NA PSG

KLABU ya West Ham inatumaini kukamilisha usajili wa mlinzi wa Paris St Germain wa Ujerumani, Thilo Kehrer, 25, kwa wakati. ***(Sky Sports)***

### SEVILLA YAIACHIA WEST HAM

KLABU ya Sevilla ambayo ilikuwa ikishindana na West Ham kumsajili Thilo Kehrer kutoka PSG, wamekubaliana ada ya euro milioni 20 na Bayern Munich kumnunua beki wa kati wa Ufaransa, Tanguy Nianzou, 20. ***(Fabrizio Romano)***

### NDOMBELE HAENDI NAPOLI

KIUNGO wa kati wa Tottenham Hotspur na Ufaransa, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 23, hatahamia Klabu ya Serie A Napoli. ***(Corriere Dello Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MANCHESTER UNITED YAMKATALIA RABIOT

**Mama na wakala wake hawaoni ni kwa nini wanapaswa kupunguza mshahara...**

**MANCHESTER,** England

MPANGO wa Manchester United ya kutaka kumnunua Adrien Rabiot umeingia dosari baada ya 'Mashetani Wekundu' hao kukataa matakwa ya Adrien Rabiot ya mshahara, kwa mujibu wa 90min.

**Rabiot alitarajiwa sana kujiunga na Man United msimu huu wa majira ya joto wakiwa tayari wamekubaliana ada ya pauni milioni 15 na Juventus kwa ajili ya mchezaji huyo.**

Hata hivyo, klabu na kiungo huyo wameshindwa kuafikiana kuhusu suala la maslahi binafsi ili kukamilisha dili hilo, huku ikifahamika kuwa kutokubali kwa Rabiot kukatwa mshahara kumeonekana kuwa tatizo kwa klabu hiyo ya Old Trafford.

Mama wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 na wakala, haoni ni kwa nini mwanawe na mteja wake wanapaswa kupunguza matakwa yake ya mshahara ikizingatiwa kwamba atapatikana kama mchezaji huru.

Rabiot alisajiliwa hapo awali na Juventus kama mchezaji huru mwaka 2019 na kwa sababu ya kukosekana kwa ada ya uhamisho, alijipatia mshahara mkubwa wa euro milioni saba kwa mwaka baada ya kodi.

Uchezaji wake haujawa wa kuvutia na klabu hiyo ikitamani sana kumbadilisha mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa msimu huu wa majira ya joto.

Njia moja ambayo Juve wanaweza kuhakikisha Rabiot hayuko kwenye orodha yao ifikapo mwishoni mwa dirisha la uhamisho ni kumuuza na Man United walionekana kuwa ndio wenye uhitaji wa mchezaji huyo.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,023

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 18 AGOSTI 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13


| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/08/22 | 19:00 | Rakow Czestochowa vs Slavia Prague | 2.73 | 3.24 | 2.53 |
| 02. 18/08/22 | 19:30 | El Gouna vs Ghazl EL Mahallah | 2.50 | 2.86 | 3.07 |
| 03. 18/08/22 | 19:30 | Al Masry Club vs Ismaily SC | 2.39 | 2.86 | 3.26 |
| 04. 18/08/22 | 20:00 | Pyunik Yerevan vs Sheriff Tiraspol | 2.83 | 3.13 | 2.52 |
| 05. 18/08/22 | 20:00 | Apollon Limassol vs Olympiakos | 3.37 | 3.22 | 2.16 |
| 06. 18/08/22 | 20:00 | CSKA Sofia vs FC Basel | 3.04 | 3.24 | 2.32 |
| 07. 18/08/22 | 20:00 | BSC Young Boys vs Anderlecht | 2.16 | 3.48 | 3.13 |
| 08. 18/08/22 | 20:00 | Maccabi Tel Aviv vs Nice | 3.02 | 3.22 | 2.33 |
| 09. 18/08/22 | 19:00 | HJK Helsinki vs Silkeborg | 2.87 | 3.22 | 2.43 |
| 10. 18/08/22 | 21:00 | SC Dnipro 1 vs AEK Larnaca | 2.63 | 3.23 | 2.63 |
| 11. 18/08/22 | 21:00 | Zrinjski Mostar vs Slovan Bratislava | 2.62 | 3.18 | 2.67 |
| 12. 18/08/22 | 21:15 | Maribor vs CFR Cluj | 3.03 | 3.13 | 2.38 |
| 13. 18/08/22 | 22:00 | Austria Vienna vs Fenerbahce | 2.78 | 3.29 | 2.46 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NUNEZ AOMBA RADHI KWA KADI NYEKUNDU LIVERPOOL



**LIVERPOOL,** England

DARWIN Nunez ameomba radhi baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu wakati Liverpool ikitoka sare ya bao 1-1 na Crystal Palace katika mchezo wa Ligi Kuu England kwenye Uwanja wa Anfield, Jumatatu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay, ambaye aliwasili kutoka Benfica kwa kitita cha pauni milioni 64, alikabiliwa na mechi ya kwanza ya kutatanisha akiwa nyumbani kwa 'Wekundu' hao, ambayo ilimalizika kwa yeye kutolewa mapema uwanjani baada ya kumpiga kichwa beki wa Palace, Joachim Andersen.

Nunez alikuwa amepiga mashuti matano - ambayo hayakulenga goli - na alimpiga kichwa Andersen baada ya kusukumwa. Mshambuliaji huyo amekuwa mchezaji wa pili wa Liverpool kutolewa katika mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu ya England; miaka 12 baada ya Joe Cole kufanya hivyo katika sare ya bao 1-1 dhidi ya Arsenal.

Na sasa Nunez ametumia ukurasa wake wa Twitter kueleza majuto yake juu ya tukio hilo, akiandika: "Ninafahamu tabia mbaya niliyokuwa nayo. Niko hapa kujifunza kutokana na makosa yangu na haitajirudia tena. Pole kwa Liverpool," alisema.



## FIFA yafuta mechi Brazil vs Argentina

**NYON,** Uswisi

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa (FIFA), limekubali kufuta mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia kati ya Brazil na Argentina.

Mchezo huo wa Septemba ulisitishwa muda mfupi baada ya kuanza wakati maofisa wa afya wa Brazil walipoingia uwanjani wakidai kuwa wachezaji wanne wa Argentina walikuwa wamekiuka sheria za kujikinga na COVID-19.

FIFA ilikuwa ikishinikiza mpambano huo kupangwa tena mwezi ujao, licha ya ukweli kwamba mchezo huo haukuwa na maana yoyote kwa sababu timu zote mbili tayari zimefuzu kwa Kombe la Dunia kule Qatar baadaye mwaka huu.

Mashirikisho ya soka ya Brazil na Argentina yote yalipinga matakwa ya FIFA, na kesi hiyo ilipelekwa katika Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo (CAS), ambapo pande zote tatu zilikubali makubaliano hayo.

Kocha Tite wa Brazil na Lionel Scaloni wa Argentina walidai kuwa hatari ya majeraha na kusimamishwa ni kubwa mno kwa mchezo huo kuchezwa, ambao ungetokea miezi miwili tu kabla ya kuanza Kombe la Dunia.

Kwa makubaliano hay timu zote za Amerika Kusi ziko huru kupanga mechi kirafiki dhidi ya wapinza wao watakaowachagua kw ajili ya maandalizi ya Komb la Dunia.

Brazil haijashinda Komb la Dunia tangu 2002 na ifedheheshwa na Ujeruma katika nusu-fainali ilipokuw mwenyeji wa michuano hiy mwaka 2014, ambapo Arge tina ilifungwa katika fainali.

Argentina wako pamoja Mexico, Poland na Saudi Ar bia katika Kundi C, huku Br zil wakiwa Kundi G pamo na Serbia, Uswizi na Came oon.

,154,178

# SIMBA QUEENS HAIKAMATIKI AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili yaliyofungwa na wachezaji wa kimataifa kutoka Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Aquino Corazone na Pambani Kuzoya yameipa timu ya Simba Queens ushindi wa mabao 2-0 jana dhidi ya She-Corporates ya Uganda kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika Ukanda wa CECAFA, hivyo kukwea kileleni mwa msimamo.

Kiungo mkabaji aliyesajiliwa msimu huu kutoka Gaspo Youth ya Kenya, akiichezea pia timu ya Taifa ya Kenya, Harambee Starlets, Aquino, alianza kuipatia timu yake bao dakika ya 22, alipoupata mpira akiwa mita zipatazo 25 hivi, akaachia shuti la chini chini lililokwenda kulia kwa kipa, Daphine Nyayenga na kujaa wavuni.

**Simba Queens ingeweza kupata mabao mengi kipindi cha kwanza kwenye mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, lakini wachezaji wake hawakuwa makini na kukosa mabao mengi.**

Kipindi cha pili, She-Corporates ilisakama lango la wenyeji wao kwa kumtumia mchezaji tegemeo, Anita Manata ambaye kwa kiasi kikubwa hakuwa na madhara sana kwenye mechi ya jana, kutokana na ukuta mgumu ulioongozwa na beki wa kati Mkongomani Daniela Nyanyanya ambaye msimu uliopita alikuwa akiichezea Yanga Princess.

Alikuwa ni kiungo mshambuliaji Pambani, raia wa DR Congo aliyepachika bao la pili dakika ya 60 kwa kichwa, baada ya kuunganisha krosi ndefu iliyopigwa na nahodha wa timu hiyo, Fatuma Issa.

Kwa matokeo hayo, Simba Queens inakwenda juu ya msimamo wa Kundi B, kwani kwenye mechi ya kwanza iliichapa GRFC ya Djibouti mabao 6-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, hivyo kuwa na pointi sita na mabao manane na haijaruhusu bao.

She Corporates ambayo kwenye mechi ya kwanza Uwanja wa Benjamin Mkapa, iliiadhibu Yei Joint Stars ya Sudan Kusini mabao 6-0, inabaki kwenye nafasi ya pili na pointi tatu, mabao sita ikiwa imeruhusu mawili.

Washindi wawili wa kila kundi watacheza nusu fainali, kabla ya kupatikana timu za kwenda fainali na bingwa atakata tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Afrika kwa Wanawake zitakazofanyika mwishoni mwa mwaka huu nchini Morocco.

KATUSUA...




Mshindi wa Jackpot Bonus ya SportPesa, Recpicius Baitwa, kutoka Moshi, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 7.9 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. **PICHA: SPORTPESA**

## *Kamati TFF sasa yakagua klabu*

**Na Adam Fungamwango**

KAMATI ya Leseni za Klabu ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), imeanza ukaguzi wa Klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kumalizana na viwanja vya Ligi Kuu.

Taarifa iliyotolewa na TFF ikisainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho hilo, Cliford Ndimbo, imeeleza kuwa ukaguzi huo unafanyika kwenye maeneo ya mpango kazi wa timu za vijana, hati ya umiliki wa viwanja au mkataba wa upangaji, sekretarieti ya klabu, mikataba ya wafanyakazi, benchi la ufundi, katiba na cheti cha usajili halisi, pamoja na hesabu za fedha zilizokaguliwa za mwaka 2021.

Kamati hiyo imehamia kwenye klabu baada ya kutoka kwenye viwanja, ambapo hivi karibuni, ilivifungia viwanja kadhaa kwa kutokidhi vigezo na kuvipitisha tisa ambavyo ndivyo kwa sasa vinatumika kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini ikakifungia kimoja, siku moja tu baada ya ligi kuanza.

Viwanja tisa ambavyo vilipitishwa ni Benjamin Mkapa, Dar es Salaam vinavyotumiwa na Simba na Yanga, CCM Kirumba, Azam Complex, Chamazi ambao ni uwanja wa nyumbani wa Azam FC, Highland Estate, Mbarali Mbeya utakaotumiwa na Ihefu, Karatu Arusha, Liti Singida utakaotumiwa na Singida Big Star, Manungu Turiani, Morogoro wa Mtibwa Sugar, Sheikh Amri Abeid, Arusha na Uhuru, Dar es Salaam.

Hata hivyo, Highland Estate nacho kimesimamishwa, baada ya mechi ya kuonekana hakifai, siku moja tu baada ya mechi ya ufunguzi.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 20/08/22 | 17:00 | Crystal Palace vs Aston Villa | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 02. 20/08/22 | 17:00 | Fulham vs Brentford | 2.39 | 3.28 | 2.93 |
| 03. 20/08/22 | 17:00 | Preston vs Watford | 2.89 | 3.14 | 2.49 |
| 04. 20/08/22 | 17:00 | Birmingham vs Wigan | 2.41 | 3.18 | 2.98 |
| 05. 20/08/22 | 17:00 | Swansea vs Luton Town | 2.41 | 3.18 | 2.98 |
| 06. 20/08/22 | 17:00 | Bolton vs Sheffield Wed | 2.85 | 3.39 | 2.39 |
| 07. 20/08/22 | 17:00 | Forest Green vs Plymouth | 2.70 | 3.40 | 2.50 |
| 08. 20/08/22 | 17:00 | Burton vs Port Vale | 2.31 | 3.38 | 2.98 |
| 09. 20/08/22 | 17:00 | Doncaster vs Salford City | 2.63 | 3.28 | 2.63 |
| 10. 20/08/22 | 17:00 | Colchester vs Leyton Orient | 2.98 | 3.33 | 2.33 |
| 11. 20/08/22 | 17:00 | Crawley Town vs AFC Wimbledon | 2.43 | 3.24 | 2.89 |
| 12. 20/08/22 | 17:00 | Mansfield vs Stockport | 2.25 | 3.49 | 2.99 |
| 13. 20/08/22 | 17:00 | Dundee Utd vs St. Mirren | 2.31 | 3.09 | 3.24 |
| 14. 20/08/22 | 17:00 | Motherwell vs Livingston | 2.25 | 3.13 | 3.33 |
| 15. 20/08/22 | 17:00 | Ross County vs Kilmarnock | 2.26 | 3.14 | 3.29 |
| 16. 20/08/22 | 17:00 | St. Johnstone vs Aberdeen | 2.93 | 2.98 | 2.58 |
| 17. 20/08/22 | 17:00 | Hamilton vs Raith Rovers | 2.43 | 3.14 | 2.99 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 18 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5610 | Vissel Kobe vs Yokohama F Marinos | 3.63 | 3.53 | 1.85 |
| 14:30 | 5070 | Dalian Aerbing vs Shijiazhuang | 2.50 | 3.24 | 2.55 |
| 15:00 | 2341 | Taraz Karatau vs Zhenis Nur-Sultan | 1.72 | 3.75 | 4.30 |
| 15:15 | 5962 | Kuala Lumpur vs Negeri Sembilan | 2.01 | 3.34 | 3.29 |
| 16:00 | 4929 | Penang vs Pahang FA | 2.36 | 3.60 | 2.65 |
| 17:00 | 3971 | Surkhon Termez vs Metallurg Bekabad | 2.80 | 2.85 | 2.55 |
| 18:00 | 4126 | Qizilqum vs Dinamo Samarqand | 1.52 | 3.73 | 5.70 |
| 18:30 | 2399 | TPS Turku vs EIF Ekenas | 1.51 | 4.12 | 5.10 |
| 18:30 | 5669 | FC Honka/Akatemia vs EPS | 1.61 | 4.14 | 4.24 |
| 19:00 | 2051 | MES Rafsanjan vs Gol Gohar | 2.65 | 2.42 | 3.24 |
| 19:00 | 4954 | Rakow Czestochowa vs Slavia Prague | 2.78 | 3.24 | 2.49 |
| 19:00 | 5623 | HJK Helsinki vs Silkeborg | 2.98 | 3.23 | 2.35 |
| 19:30 | 2709 | El Gouna vs Ghazl EL Mahallah | 2.44 | 2.86 | 3.16 |
| 19:30 | 4867 | Ferencvaros TC vs Shamrock Rovers | 1.47 | 4.35 | 6.28 |
| 19:30 | 5531 | Al Masry Club vs Ismaily SC | 2.17 | 2.91 | 3.71 |
| 20:00 | 1036 | Malmo vs Sivasspor | 1.80 | 3.58 | 4.23 |
| 20:00 | 1308 | Pyunik Yerevan vs Sheriff Tiraspol | 3.13 | 3.13 | 2.32 |
| 20:00 | 1785 | Hapoel Acre vs Ironi Tiberias | 1.92 | 3.24 | 4.15 |
| 20:00 | 2096 | CSKA Sofia vs FC Basel | 3.12 | 3.32 | 2.23 |
| 20:00 | 2179 | Rigas Futbola Skola vs Linfield Belfast | 1.68 | 3.53 | 5.25 |
| 20:00 | 2383 | BSC Young Boys vs Anderlecht | 2.05 | 3.63 | 3.27 |
| 20:00 | 2943 | Hapoel Afula vs El Fahem | 2.37 | 3.33 | 2.88 |
| 20:00 | 3381 | Slovacko vs AIK Football | 1.95 | 3.44 | 3.74 |
| 20:00 | 3749 | Hapoel Ramat Gan vs Maccabi Jaffa | 2.52 | 3.02 | 2.92 |
| 20:00 | 3883 | Maccabi Tel Aviv vs Nice | 2.93 | 3.23 | 2.38 |
| 20:00 | 5305 | FC Zurich vs Hearts | 1.86 | 3.63 | 3.88 |
| 20:00 | 5523 | Apollon Limassol vs Olympiakos | 3.33 | 3.23 | 2.18 |
| 20:00 | 5695 | Molde vs Wolfsberger AC | 1.66 | 3.99 | 4.64 |
| 20:30 | 2029 | Universitatea Craiova vs Hapoel Beer Sheva | 2.05 | 3.39 | 3.49 |
| 20:45 | 1179 | Basaksehir vs Royal Antwerp | 2.04 | 3.37 | 3.52 |
| 20:45 | 2712 | Ludogorets Razgrad vs Zalgiris | 1.44 | 4.43 | 6.65 |
| 21:00 | 1579 | FC Vaduz vs Rapid Vienna | 3.99 | 3.74 | 1.81 |
| 21:00 | 2056 | SC Dnipro 1 vs AEK Larnaca | 2.57 | 3.18 | 2.73 |
| 21:00 | 4957 | Throttur Vogum vs Grotta | 3.78 | 3.88 | 1.73 |
| 21:00 | 4974 | Zrinjski Mostar vs Slovan Bratislava | 2.77 | 3.12 | 2.57 |
| 21:15 | 1241 | Maribor vs CFR Cluj | 3.33 | 2.98 | 2.30 |
| 21:30 | 1231 | KAA Gent vs Omonia Nicosia | 1.33 | 5.07 | 8.32 |
| 21:30 | 2018 | Lech Poznan vs Dudelange | 1.26 | 5.65 | 10.08 |
| 21:30 | 3488 | FC Koln vs Videoton FC | 1.27 | 5.26 | 11.14 |
| 21:30 | 5197 | Steaua Bucuresti vs Viking | 1.83 | 3.62 | 4.03 |
| 21:45 | 2346 | Villarreal vs Hajduk Split | 1.27 | 5.48 | 10.14 |
| 21:45 | 5017 | West Ham vs Viborg FF | 1.23 | 5.87 | 11.13 |
| 22:00 | 1126 | AZ Alkmaar vs Gil Vicente | 1.58 | 4.03 | 5.25 |
| 22:00 | 2291 | Partizan vs Hamrun Spartans | 1.19 | 6.08 | 16.21 |
| 22:00 | 2624 | Shkupi Skopje vs KF Ballkani | 2.17 | 3.24 | 3.34 |
| 22:00 | 3225 | Coca Cola vs Ceramica Cleopatra | 2.04 | 3.17 | 3.72 |
| 22:00 | 4525 | Fiorentina vs Twente | 1.51 | 4.25 | 5.86 |
| 22:00 | 4970 | Austria Vienna vs Fenerbahce | 3.08 | 3.33 | 2.24 |
| 22:15 | 3747 | Fylkir vs UMF Selfoss | 1.31 | 5.29 | 6.67 |
| 23:00 | 1028 | FC Aguablanca vs Tigres FC (COL) | 2.47 | 2.81 | 2.95 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Agosti 18, 2022

Nipashe




**United yamkatalia Rabiot** UKURASA 21

CHA PILI...



Mshambuliaji wa Simba, Moses Phiri (kushoto), akishangilia sambamba na Pape Sakho, baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Geita Gold FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Nabi awapa Aziz Ki, Morrison miezi mitatu

**Na Saada Akida**

LICHA ya kucheza mechi mbili za kimashindano, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema kwa sasa babo hawezi kutoa tathimini ya ubora wa wachezaji wake wapya na badala yake anawapa muda wa miezi miwili hadi mitatu.

Wachezaji wapya wa Yanga ambao imewasajili msimu huu ni Aziz Ki raia wa Burkina Faso, Mrundi Gaël Bigirimana, Mghana Bernard Morrison, Joyce Lomalisa (DR Congo) na Lazarous Kambole raia wa Zambia ambaye hajacheza mechi hata moja ya mashindano.

Mchezo wa kwanza wa mashindano, Yanga iliibuka na ushindi mabao mawili dhidi ya Simba kwenye Ngao ya Jamii kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi iliyopita kabla ya juzi kupata matokeo kama hayo dhidi ya Polisi Tanzani katika mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu msimu huu iliyopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha shukran kwa Fiston Mayele na Bakari Mwamnyeto waliocheka na nyavu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema kutokana na kutopata maandalizi mazuri ya msimu mpya (Pre-Season), hawezi kutoa tathmini ya wachezaji wake wapya na anawapongeza nyota wake kwa kupambana kutafuta matokeo.

“Kwa sasa ni mapema kutoa tathmini za wachezaji wangu wapya na nimewapa muda wa miezi miwili hadi mitatu baada ya hapo ndiyo naweza kutoa tathimini kwa sababu watakuwa wameshazoeana na kutengeneza muunganiko mzuri na wachezaji waliowakuta,” alisema Nabi.

Kuhusu mchezo dhidi ya Polisi Tanzania, alisema ulikuwa mgumu na kwamba misimu yote wanapokutana na Polisi Tanzania inakuwa mechi ngumu kutokana na wapinzani wao hao kucheza soka la kujilinda zaidi.

# Simba yaanza ligi kileleni

## ●●● Okrah aonyesha mambo makubwa akifungua akaunti ya mabao na Phiri, huku Chama...

**Na Adam Fungamwango**

AUGUSTINE Okrah kiungo wa Kimataifa wa Ghana, na straika kutoka Zambia, Moses Phiri, jana walifungua akaunti zao za mabao wakicheza kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na Klabu ya Simba, waliyoiwezesha kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Mzambia mwingine, Clatous Chama, alifunga bao la tatu lililoiweka timu hiyo kileleni mwa msimamo kabla ya mechi nyingine ya Ligi Kuu jana usiku kati ya Azam FC na Kagera Sugar.**

Okrah, aliyesajiliwa msimu huu akitokea Bechem United ya Ghana, aliingia dakika ya 34 ya mchezo kuchukua nafasi ya Jonas Mkude, na kutumia dakika mbili tu kuwamo uwanjani kabla ya kupachika bao hilo kwa mpira ‘uliokufa’ (faulo).

Faulo hiyo ilitokana na Chama kufanyiwa madhambi nje kidogo ya eneo la hatari, ambapo Okrah aliachia shuti kali la mguu wa kushoto ambalo kipa Sebusebu Samson pamoja na kuuchupia mpira huo kutaka kuukamata, lakini ulikuwa na kasi mno, hivyo ukamshinda kabla ya kujaa wavuni.

Mechi ilianza kwa Simba kuutawala mpira kwa dakika 20 za mwanzo, huku Peter Banda akikosa bao dakika ya saba tu, baada ya kutanguliziwa mpira na Phiri, mchezaji mpya alisajiliwa kutoka Zanaco ya Zambia, lakini shuti lake dhaifu liliishia kwenye mikono ya Sebusebu.

Mshindi wa Kiatu cha Dhahabu wa msimu uliopita, George Mpole nusura aipatie timu yake bao dakika ya 28 ya mchezo, alipopiga faulo iliyodunda, lakini kwa bahati nzuri haikumpoteza maboya Kipa wa Simba, Aishi Manula ambaye alirejea langoni, baada ya kutocheza mechi nyingi za mwisho wa msimu uliopita na za mwanzo.

Banda kama angetulia, angeweza kuipatia Simba bao dakika ya 31, lakini shuti lake la krosi aliyounganisha kutoka kwa Shomari Kapombe ikatoka nje.

Alikuwa ni Banda, aliyeambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto na kumega pande safi kwa Chama, ambaye alimchungulia Mzambia mwenzake, akapiga krosi fupi ya upendo ambayo Phiri alichofanya ni kuweka mguu tu kuugusa mpira uliokwama wavuni dakika ya 61.

Licha ya timu zote kufanya mabadiliko, lakini kipindi cha pili Geita Gold ilionekana kutawala zaidi hasa baada ya Simba kupata bao la pili, lakini mastraika wake, Mpole na Daniel Lyanga walidhibitiwa na walinzi wa Simba waliokuwa wakiongozwa na Mohamed Ouattara.

Almanusura Geita Gold ipate bao dakika ya 79, kabla ya shuti la Mpole kumbabua Sadio Kanoute na kurejea uwanjani.

Simba ilifanya shambulizi la kushtukiza, pale Okrah alipowafungasha tela mabeki wa Geita Gold FC, kabla ya kumuangusha ndani ya eneo la hatari, hali iliyosababisha mwamuzi Ahmed Aragija kuamuru upigwe mkwaju wa penalti.

Chama alichukua jukumu hilo na kuweka mpira ndani ya kamba, akiandika bao la tatu dakika tisa kabla ya mechi kumalizika.

Kwa matokeo hayo, Simba kabla ya mechi ya jana, inaongoza ligi ikiwa na pointi tatu na mabao matatu, ikifuatiwa na Mbeya City iliyoichapa Dodoma Jiji FC mabao 3-1 jana, ikiwa kwenye nafasi ya pili, Yanga ambayo ilishinda mabao 2-1 juzi ikiwa kwenye nafasi ya tatu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >